# Nipashe

Jumamosi Machi 30, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581631

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US


**Mwarobaini** vifo vitokanavyo na ulaji wa kasa wapatikana UKURASA 5

**Lipa** kwa namba hii' yawapeleka jela miaka mitatu UKURASA 5

**ACT** yapendekeza mambo matano kumaliza tatizo la maji nchini UK. 4



DI MARIA ATISHIWA KIFO UKURASA 21

## IBADA IJUMAA KUU

# Maaskofu watema nyongo

UKURASA 2



Askofu Beatus Kinyaiya

Askofu Dk. Dickson Chilongani

Askofu Stanley Hotay

Askofu Liberatus Sangu

Askofu Mkuu Isaack Amani

Vijana wakimsulubisha kijana Andrew Clement, aliyeigiza kama Yesu wakati wa igizo la kumbukizi ya mateso ya Yesu Kristo, wakati wa Ibada ya Ijumaa Kuu katika Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria Mpalizwa Mkwawa, mjini Iringa jana. **Picha zaidi Uk. 7. PICHA: FRANCIS GODWIN**

## Baba wa binti aliyeuawa, kufukiwa ndani aleza machungu

UKURASA 4

## RIPOTI YA CAG

# Wadau wataka hatua zichukuliwe, waonyesha shaka uhai wa NHIF

UKURASA 4


**MICHEZO** YANGA, MAMELODI MECHI YA KISASI UK.24

**MAONI,** UK.6

# Maaskofu watema cheche Ijumaa Kuu

Na Waandishi Wetu



Vijana wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), wakiigiza kuteswa kwa Yesu Kristo, katika Kanisa la Azania Front, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

MAASKOFU, mapadri na wachungaji wa madhehebu ya dini, jana walitoa ujumbe kwa serikali na jamii katika ibada za Siku ya Ijumaa Kuu zilizofanyika katika makanisa mbalimbali nchini.

Miongoni mwa mambo waliyoibua ni wananchi kuacha kuchagua wabadhirifu katika uchaguzi ujao huku viongozi wa serikali na taasisi zake wakitakiwa kutomwangusha Rais Samia Suluhu Hassan.

Pia walikemea viongozi wa umma wenye tabia za ubinafsi, ufisadi, usaliti na upendeleo pamoja na vitendo vya kikatili dhidi ya watoto, wanawake na wanandoa vinavyoendelea na hata kusababisha vifo.

Sambamba na hayo, wametaka kila mwenye uwezo, sifa na hofu ya Mungu akagombee nafasi mbalimbali katika chaguzi hizo.

**ACHENI KUJIUA**

Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu Dodoma, Beatus Kinyaiya, alikemea watu ambao wamekuwa wakikata tamaa kwenye maisha na kufikia hatua ya kutaka kujiua kwa kisingizio cha ugumu wa maisha, kuacha na kumwamini Mungu.

Akizungumza katika ibada ya kitaifa iliyofanyika katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Paulo wa Msalaba, Askofu Mkuu Kinyaiya alisema watu hawapaswi kukata tamaa licha ya magumu wanayoyapitia katika maisha bali waendelee kumwomba Mungu kila wakati.

Askofu wa Kanisa katoliki Jimbo la Shinyanga, Mhashamu Liberatus Sangu, aliwataka watu wenye tabia ya kujinufaisha kupitia shida za wengine kwa kujipatia mali na heshima, kuacha vitendo hivyo, badala yake wawe mstari wa mbele kuwasaidia wenye uhitaji.

Paroko wa Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Theresia Barabara 20, jijini Tanga, Padre Joseph Mbena, alisema jamii inapaswa kuacha vitendo viovu vikiwamo kutupa watoto na kutekeleza familia jambo ambalo linasababisha maumivu kwenye ndoa.

Mchungaji Kiongozi wa Kanisa Kuu la Kanisa la Kiinjili Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Dodoma, Daniel Sailowa, aliwataka wateule wa Rais Samia kutomwangusha katika utendaji kwa kushughulikia kero za wananchi katika maeneo yao.

Alisema bado kuna baadhi ya maeneo yanakabiliwa na kero kwenye afya, elimu, miundombinu."Hawa watendaji wakiyasimamia maeneo yenye kero kwa Watanzania itaongeza imani kwa Rais na serikali yake. Pamoja na Rais kufanya kazi kwa uaminifu na kwa vitendo kwa malengo ya kuwafikia wananchi, bado kuna baadhi ya watendaji wanakwamisha utendaji huo na Watanzania walio wengi wanashindwa kupata maendeleo," alisema.

Aidha, Mchungaji Sailowa aliwakumbusha watanzania kuwakumbuka wafungwa waliofungwa magerezani kwa kuwapatia misaada mbalimbali itakayowafariji.

Akitoa salamu katika ibada hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, aliwataka waamini wa Kikristo kuombea uchaguzi wa serikali za mitaa pamoja na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Alisema katika uchaguzi, kila mtu ana haki ya kuchagua na kuchaguliwa, hivyo kila mtu ajiandae ili kupata viongozi bora. Aliwahimiza wananchi mkoani Dodoma kusherehekea sikukuu ya Pasaka kwa amani na kila mtu ahakikishe wanasaidia kulinda amani iliyopo.

Mkuu wa Jimbo la Babati wa Kanisa la Kinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Mchungaji Robert Mallya, alikemea ndoa za jinsia moja, unyanyasaji na kupenda fedha bila kufanya kazi.

**WAHITAJI WAKUMBUKWE**

Askofu wa Kanisa la Anglikana Tanzania Dayosisi ya Kati (DCT), Dk. Dickson Chilongani, aliwaomba watanzania wenye kipato kuwakumbuka watu wenye uhitaji wakiwamo wajane, yatima, wenye ulemavu na watoto walio kwenye vituo vya malezi.

Katika mahubiri yake iliyoambatana na kutoa mchango kwa watoto wanaosoma Shule ya Msingi Wasioona ya Buigiri iliyoko wilayani Chamwino, Dk. Chilongani alisema mara nyingi watoto hao na wale wasioijweza wamekuwa wakitengwa na kusahaulika.

"Yesu mwenyewe alionyesha upendo kwa watu wote na hakubagua, hivyo na sisi watanzania tunatakiwa kuwa na moyo huo wa kuwapenda na kuwasaidia watu wenye uhitaji,"alisema.

**WAKEMEA UFISADI**

Makamu Mwenyekiti wa Umoja wa Makanisa mkoani Arusha, (UKAMA), Askofu Isaac Amani, alionya wananchi kuchagua viongozi wabadhirifu, wabinafsi, wenye siasa za upendeleo katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu ujao.

Askofu Isaac ambaye ni Askofu Mkuu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Arusha, alitoa onyo hilo wakati wa ibada ya Ijumaa Kuu ya UKAMA iliyofanyika viwanja vya Shekhe Amri Abeid, ikitanguliwa na maandamano kutoka madhehebu 13 ya makanisa mbalimbali. Pia alionya vitendo vya kikatili, vinavyoendelea dhidi ya watoto na kwa wanandoa na kusababisha vifo na kukemea baadhi ya viongozi wa umma wenye tabia za ubinafsi, ufisadi, usaliti na upendeleo.

"Wananchi lazima tutumie akili kuchagua viongozi wenye sifa, wakweli na wanaosimamia siasa safi ambazo si za matusi na wasio na tamaa ya mali pia wawe na hofu ya Mungu.

"Ili kuwapata viongozi hawa, lazima wananchi tujitokeze kwa wingi kujiandikisha kwenye Daftari la Wapigakura ili tupate haki ya kuchagua viongozi waadilifu na wenye hofu ya Mungu.

"Tunachagua viongozi wa aina gani? Tunapiga kura tukiangalia nini? Ukwasi wao au uwezo wao wa kutuongoza? Tuchague viongozi tunaowajua kwa tabia na tunaoishi nao katika maeneo yetu," alisema.

Kuhusu ukatili kwa watoto na wanandoa, Askofu Amani alisema ufike wakati sasa wanaofanya vitendo hivyo wabadilike kama Yesu alivyojitoa kafara kwa ajili ya maisha yao.

Aidha, aliwaonya baadhi ya vijana wanaojifanya kwenda na wakati kwa kujiingiza katika ulevi wa pombe, dawa za kulevya, makundi hatarishi na matumizi mbaya ya mitandao na kuwataka waache kwa kuwa wanajifungia milango yao mbinguni.

Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mount Kilimanjaro, Dk. Stanley Hotay, ambaye pia ni Mwenyekiti wa UKAMA, alisema hivi sasa kuna tabia ya wizi jijini Arusha na kuomba vyombo vya ulinzi na usalama viendelee kuimarisha ulinzi hasa katika kipindi cha sikukuu za Pasaka.

"Mwaka huu ni muhimu wa uchaguzi. Kila mtu mwenye uwezo na sifa akagombee hatuwezi komesha rushwa, lazima watu wawe waadilifu, na lazima watu wakagombee walio na hofu ya Mungu,"alisema.

**IMEANDALIWA na Paul Mabeja, Peter Mkwavila na Ibrahim Joseph (DOM), Cynthia Mwilolezi (ARUSHA), Marco Maduhu (SHINYANGA), Oscar Assenga (TANGA), Mary Mosha (Moshi), Jaliwasson Jasson (MANYARA) na Vitus Audux (MWANZA)**

TANGAZO


Nipashe
MWANGA WA JAMII
Baada ya muda sasa...
Jambo letu hili hapa!!
iPP
CARES FOR YOU
The Guardian
www.ippmedia.com

HABARI KITAIFA



Mkurugenzi wa Jumuiya ya kuhifadhisha Quran, Shekhe Athumani Kapolo (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam juzi, kuhusu mashindano ya kuhifadhi Quran ya Kimataifa yatakayofanyika kesho Diamond Jubilee. Kushoto ni Mratibu wa mashindano hayo, Mtoro Bakari na Mkurugenzi Mkuu wa Itifaki Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Mohamed Amran. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wadau wataka hatua ripoti ya CAG

**Na Waandishi Wetu**

SIKU moja baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuwasilisha ripoti ya ukaguzi kwa mwaka 2022/23, wadau wameishauri serikali kuchukua hatua kwa mashirika ambayo yamekuwa yakiendelea kupata hasara,.

Sambamba na hayo, wadau hao wameonyesha shaka kuhusu uhai wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF).

Aidha, wamesema ni wakati mwafaka wa kubadili sheria kwa kuanzia na sheria mama (Katiba) ili kusaidia kuleta uwajibikaji zaidi na kulinda rasilimali.

Mchambuzi wa masuala mbalimbali na Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU), Dk. Paul Loisulie, alisema kujirudia kwa taarifa za ubadhirifu hasa kwa baadhi ya mashirika ni jambo linalochosha na kuchefua.

"Inaleta mazoea kwamba hayo mashirika yasipotajwa ripoti hainogi, ifike wakati serikali ichore mstari wa kuvumilia hasara inayojitokeza kila mara CAG anapotoa ripoti.

"Hii itasaidia kuokoa rasilimali zetu na kuondokana na mawazo ya kubinafsisha kwa imani kwamba ufanisi na tija, zitafikiwa,"alisema nak ushauri watumishi wa umma kuamka usingizini kwa kuwa ni sehemu ya mchango mkubwa wa hasara inayoshuhudiwa serikalini.

"Tusipoamka mashirika yetu yataendelea kubinafsishwa na sisi kubaki kuwa watazamaji. Wakati wa kuchukua hatua ni sasa, ni wakati muafaka pia, kubadili sheria zetu tukianza na sheria mama (Katiba), hii itasaidia kuleta uwajibikaji zaidi na kulinda rasilimali," alisema.

Kuhusu NHIF, Dk. Loisulie alisema ni jambo lililoibua mkanganyiko na mshtuko zaidi kwa wanufaika.

"Watu wanazidi kupoteza imani na matumaini kwa NHIF. Kinachowashikilia watu mpaka sasa wabaki NHIF ni ubabe (matakwa) ya kisheria. Laiti watu wangeruhusiwa kuchagua mfuko wa bima, basi NHIF ingebakiwa na wanachama wachache sana," alisema.

Alibainisha kuwa taarifa ya NHIF inaonyesha pia kwamba safari ya kuelekea kwenye mpango wa bima ya afya kwa wote ni ndefu na yenye milima na mabonde.

Hata hivyo, alisema pamoja na kuongezeka kwa hati safi ni kiashiria cha kwamba wahusika (taasisi) zimeongeza uelewa katika taratibu za mipango na kifedha.

"Uelewa huo si lazima iwe ni uthibitisho kwamba hakuna upigaji. Watu wanaweza kufuata taratibu zote, lakini bado wakachepusha rasilimali kwa maslahi binafsi," alisema.

Naye Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dk. Abdallah Seni, alisema kuna tatizo la usimamizi kwa mashirika ambayo yameonekana kwenye ripoti ya CAG kujiendesha kwa hasara na kushauri kwenda kujifunza kwenye nchi zingine zenye mashirika ya aina hiyo uendeshaji wake.

"Ni vizuri kutafuta uzoefu kwenye nchi zenye mashirika kama haya zinazofanya vizuri, hii itasaidia kuondokana na tatizo la hasara kila ripoti ya CAG inapotolewa mashirika mengine yamekuwa kama ni desturi kuonekana kuisababishia hasara serikali," alisema.

Dk. Sei alitaka wale wanaopewa dhamana ya kusimamia mashirika hayo kujielimisha kwa kina ili kuleta ufanisi kwenye taasisi zao.

Mkazi wa Dodoma, Tusekelege Mbamba, alisema kuna tatizo la magonjwa ya afya ya akili katika jamii na kwamba, ushauri wa CAG uzingatiwe ili kupata huduma za utengamano.

Hussein Kivambe, mkazi mwingine wa Dodoma, alisema afya ya akili ni tatizo linalokuwa na serikali iongeze vituo vya kutoa huduma, lakini kuongeza utambuzi kwa kuwa na wataalamu wa kutosha kufikia ngazi ya chini ya jamii.

Alisema huduma za kisaikolojia bado haziwafikii watu wengi na kusababisha wengine kuathiriwa zaidi na kufikia hatua ya kufanya matukio ya kujidhuru.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo ya Wajasiriamali (IMED), Dk. Donath Olomi, alisema ubadhirifu huo unathiri nchi kwa kupoteza rasilimali fedha ambazo zingepaswa kuwekezwa kwa ajili ya miundombinu ambayo ingesaidia kutatua changamoto nyingine mbalimbali kama miradi ya afya na elimu. "Unaposikia kila wakati watu wameiba fedha za umma, inajenga utamaduni wa wafanyakazi waadilifu kuona upigaji ni jambo la kawaida.

"Inatakiwa hatua zinazochukuliwa ziwekwe wazi ili kila Mtanzania ajue ni hatua zipi zimechukuliwa. Wakati mwingine ripoti zinapotolewa, Mkaguzi (CAG) akikuta fedha zimetumika kinyume haelezi mazingira ya utumikaji wake, yeye anaripoti alichokikuta.

"Kwa hiyo unaweza ukakuta kuna fedha ilitolewa kwa kauli ya kiongozi na kupelekwa sehemu nyingine ya mradi, lakini CAG hawezi kufuatilia hilo kwa sababu si kazi yake. Ninashauri kunapotokea taarifa yenye maelekezo tofauti, kutolewe taarifa kwamba jambo lile liliiloripotiwa hivi liko hivi," alisema.

Alipoulizwa kuhusu hasara ya Sh. bilioni 156 ya NHIF, alisema inaupunguzia mfuko uwezo wa kujisimamia na athari yake ni kwamba kazi ya kumsaidia mtu anayeuumwa inapungua na wakati mwingine inamlazimu mgonjwa kutumia fedha zake za mfukoni kununua dawa.

Alisema hilo ni jambo linaloathiri uchumi wa mtu binafsi na kwamba, ili kuziba mianya ya upigaji fedha, serikali inapaswa kuwawajibisha waliokumbwa na kashfa. Kuhusu afya ya akili, Dk. Olomi alisema jamii inaathirika sana na kuathiri kipato cha wananchi mmoja mmoja kutokana na tabia za matokeo tatizo hilo.

"Wakati mwingine hata upigaji wa fedha unachangia na watu wenye afya ya akili na kwamba, kuna wakati mtu anapiga fedha mpaka unajiuliza huyu ana akili timamu kweli?" alihoji.

**Imeandaliwa na Ibrahim Joseph (DODOMA) na Halfan Chusi (DAR)**

# ACT Wazalendo yapendekeza mambo matano kumaliza tatizo la maji nchini

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimetoa maopendekezo Matano kwa serikali ili kukabiliana na tatizo la upatikanaji wa uhakika wa maji safi na salama ikiwamo kuongezewa bajeti kuanzia mwaka ujao wa fedha.

Imesema kuanzia mwaka wa fedha 2024/25, serikali haina budi kuongeza bajeti katika sekta ya maji angalau kufikia asilimia tano ya bajeti ya serikali kwa miaka mitano mfululizo ili kumaliza kabisa tatizo hilo.

Taarifa ya chama hicho iliyotolewa jana na Waziri Kivuli wa Maji, Yasinta Awiti, ilitaja hatua nyingine kuwa ni Wizara ya Maji kuwawajibisha watumishi wazembe wote wanaosababisha kuchelewa kwa miradi na kufanya ubadhirifu wa fedha za umma. "Tunaitaka serikali iimarishe mfuko wa taifa wa maji kwa kuupa chanzo cha uhakika cha mapato," alisema.

Pia alisema serikali itoe ruzuku kwa mamlaka za maji ili kuziwezesha kupanua na kuboresha miundombinu ya maji katika maeneo yao pamoja na kusimamia. Kadhalika, kusimamia huduma za maji zinazotolewa na watu binafsi ili kudhibiti usalama wa maji na gharama za huduma hiyo. Awiti alisema kwa muda mrefu wameshuhudia vilio vya wananchi wakilalamikia mgao wa maji usiokwisha bila kujali wakati wa mvua ama kiangazi au kutopatikana kabisa kwa maji safi na salama, hasa maeneo ya vijijini. "Tumeshuhudia serikali ikitenga bajeti kiduchu ya kuwekeza kwenye uzalishaji, usambazaji na uendelezaji wa huduma ya maji.

"Mfano kwa miaka mitatu mfululizo tumeona uwiano wa bajeti ya maji kwa bajeti ya serikali ukiendelea kushuka kutoka asilimia 2.2 mwaka 2021 hadi asilimia 1.7 mwaka 2023," alisema.

Pia alisema takwimu zinaonyesha zaidi ya vijiji 3000 havijaunganishwa kabisa na huduma ya maji ukiachilia vile vilivyounganishwa lakini hakuna huduma.



Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera (kulia), akipima kwa futi lango la uzio wa jengo la bweni la watoto wenye mahitaji maalum wa Shule ya Msingi Songambele, kata ya Mirerani, wakati akikagua ujenzi huo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Baba wa binti aliyeuawa kisha kufukiwa chumbani afunguka

**Na Beatrice Shayo**

BABA mzazi wa marehemu Beatrice Mgongolwa (32), Mzee Talius Mgongolwa, ambaye mwanawe anadaiwa kuuwawa na kufukiwa katika chumba alichokuwa anaishi na mwanamume, ameeleza namna alivyomtafuta binti yake zaidi ya mwaka bila mafanikio. Mauaji hayo yanadaiwa kufanywa na mwanamume wake, Januari Mosi, mwaka huu, katika Kijiji cha Kimamba A, Wilaya ya Kilosa, mkoani Morogoro, na kugundulika mwezi Machi 22, mwaka huu.

Mgongolwa akizungumza na mwandishi wa habari hii, alisema tangu Machi, 2022, alikuwa anamtafuta binti yake bila mafanikio.

Alisema alifanya jitihada mbalimbali za kumtafuta mtoto wake ikiwamo kutoa taarifa Kituo cha Polisi cha TPC, kilichoko kijiji wanachoishi cha Magogini mkoani Kilimanjaro bila mafanikio.

Mgongolwa alisema baada ya taarifa hiyo polisi walienkdelea kumtafuta katika vijiji vya karibu na eneo analoishi hakufanikiwa kupata taarifa kwa zaidi ya mwaka.

"Hakuwa na simu ndio maana nilikuwa ninapata shida ya mawasiliano naye. Mwaka jana nilikata tamaa nikasema basi huko alipo siku moja atarudi maana anapajua nyumbani. "Nimemtafuta sana tatizo hakua na namba za simu. Hatimaye taarifa ya kifo cha binti yangu nikazipata kupitia kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi ya Mselesi iliyoko Wilaya ya Moshi Vijijini, mkoani Kilimanjaro.

"Binti wa marehemu aliulizwa huko Kilosa mlikuwa mnakaa kijiji gani (Moshi) akawajulisha na shule aliyokuwa anasoma ndipo wakamtafuta Mwalimu Mkuu wa Shule hii.

"Mwalimu Mkuu naye aliulizwa kama anaifahamu familia ya marehemu (binti yangu) ndipo alipokwenda kwa Mtendaji wa Kijiji kuniulizia akapatiwa namba zangu akanipigia simu akaniambia ninahitajika kwa huyo mwalimu," alisema. Alisema wakati akipokea taarifa hizo alikuwa katika shughuli zake za kilimo na alipoitikia wito ndipo alipoelezwa habari za kifo cha mtoto wake. "Tukio hilo lilinishtua nikajiandaa kwenda Kilosa ambapo zilifanyika taratibu na kunipatia mabaki ya mwili wa marehemu na kuzika Machi 25, mwaka huu," alisimulia.

Alisema awali (binti yake) ambaye ni wa pili kuzaliwa kati ya watoto wanane alionao, alikuwa akifanya kazi katika kiwanda cha sukari cha TPC kilichoko mkoani Kilimanjaro. Baada ya kugundulika kwa mauaji hayo Machi 22, mwaka huu, siku tano mbele mtuhumiwa huyo alifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi mkoani Morogoro akikabiliwa na mashtaka manne. Mashtaka hayo ni kuua, kubaka, kuwachoma watoto na vitu vyenye ncha kali katika miili yao ikiwamo sehemu za siri.

# Mwarobaini vifo vitokanavyo na ulaji wa kasa wapatikana

**Na Jenifer Gilla**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imezindua Mpango wa Taifa wa Kuhifadhi Kasa wa Baharini wa miaka mitano ili kudhibiti kuvuliwa kinyume cha Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 na nyama yake kuliwa na binadamu, hivyo kusababisha vifo.

Uzinduzi huo umefanyika ikiwa ni takribani wiki tatu tangu kuripotiwa taarifa ya watu tisa kufariki dunia na 98 kuwa na hali mbaya baada ya kula nyama ya kasa katika eneo la Kisiwapaza, Kusini Pemba, Zanzibar.

Akizindua mpango huo juzi wilayani Mkuranga, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema umeandaliwa ili kuongeza kasi ya kumlinda kiumbe huyo kwa kuwa, Sheria ya Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu na Kanuni za Uvuvi mwaka 2009, zimemuainisha kuwa miongoni mwa walio hatarini kutoweka.

Alisema licha ya kanuni za uvuvi kupiga marufuku shughuli zozote za uvunaji wa kasa hai vitendo hivyo vimeshamiri kwa lengo la kuuza nyama yake, ingawa wanaokula hupata madhara ya kiafya na wengine kufariki dunia.

"Kiumbe huyo si chakula bali ni kivutio kikubwa cha watalii ambao hupenda kuwaona wakiwa hai hususani wanapototoa mayai. Watafiti pia huwatumia kukuza maarifa juu ya mchango wake katika ikolojia na namna ya binadamu wanavyoweza kunufaika na uwapo wake. Ulega alisema kupitia filamu ya The Royal Tour, Rais Samia Suluhu Hassan amekuza utalii wa baharini kwa kuongeza idadi ya watalii kutoka 27,987 mwaka 2021 hadi 40,088 mwaka 2023. Alisema hali hiyo mechangia kukuza pato la taifa na uchumi wa nchi, hivyo viumbe hao wasipolindwa watatoweka na kurudisha nyuma juhudi za kiongozi huyo.

Alisema kwa kutambua hilo, Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) katika wizara yake kwa kushirikiana na wadau wakiwamo mashirika yasiyo ya kiserikali ya Sea Sense, WWF na USAID Tuhifadhi Maliasili, wanaendelea kutoa elimu kwa jamii za Pwani juu ya uhifadhi na kuhamasisha wadau kutumia mpango huo kulinda viumbe hao.

Mkurugenzi wa Seasense, Gozbert Katunzi, alisema walifanikiwa kuandaa mpango huo wa mwaka 2004 hadi 2009 kwa kushirikiana na Shirika la USAID Tuhifadhi Maliasili na kupata fedha kutoka Serikali ya Marekani.

"Uandaaji wa mpango wa kitaifa ulihusisha wanajamii, idara za serikali, sekta binafsi na wadau wengine mbalimbali kutoka Tanzania bara na Zanzibar,"alisema.

Alisema kwa miaka 20 shirika hilo limekuwa likifuatilia mienendo ya viumbe walio katika hatari kubwa ya kutoweka akiwamo kasa wa baharini na nguva na takwimu zinazokusanywa zimekuwa zikitumika kuandika taarifa mbalimbali zinazohusu viumbe hao. Naibu Msimamizi wa Mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili, Exper Pius, aliwahimiza wadau wa uhifadhi kuunga mkono juhudi za serikali katika kuutekeleza mpango huo ili kulinda viumbe wa bahari.

Alisema rasilimali bahari ikiwamo kasa wa baharini wanakabiliwa na tishio kubwa la kutoweka linalotokana na uvunaji usiozingatia sheria na kanuni, hivyo mpango huo ukitekelezwa ipasavyo watakuwa salama.

Mhifadhi Mkuu wa MPRU, Dk. Godfrey Mpungura, alisema mpango huo umeainisha mikakati yenye malengo mbalimbali ikiwamo kupunguza sababu za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja za vifo vya kasa wa baharini. Alisema unalenga pia kupunguza uharibifu wa makazi ya viumbe hao na kuhamasisha uwapo wa programu mbalimbali za kutoa elimu ya uhifadhi wa kasa katika jamii zinazoishi katika pwani ili kuendelea kuwatunza.

# Wafungwa miaka mitatu kisa 'lipa kwa namba hii'

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imewahukumu wakazi 11 wa Ifakara mkoani Morogoro kifungo cha miaka mitatu jela au kulipa faini ya Sh. milioni sita kila mmoja, baada ya kupatikana na hatia ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutoa taarifa za uongo mtandaoni.

Washtakiwa hao ni Fredrick Kanepela, Julius Mwabula, Amiry Luwiso, Tareeq Sadrudin, Ashraf Awadhi, Frank Kifyoga, Samson Tandike, Michael Haule, Mussa Maganga, Helman Lwambano na Kelvin Mkapila.

Hukumu hiyo ilitolewa Machi 26, mwaka huu, na Hakimu Mkazi Mwandamizi Annah Maguta, baada ya washtakiwa hao kusomewa na kukiri mashtaka yanayowakabili.

Hakimu Maguta alisema hukumu hiyo imetolewa kwa washtakiwa 11 kati ya 23 wanaokabiliwa na kesi hiyo.

Alisema washtakiwa hao 11 waliohukumiwa waliomba kuingia makubaliano ya kumaliza kesi kwa kukiri makosa yao yaani 'pre bargain'.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao na jopo la mawakili wa serikali ambao ni Neema Moshi, Royda Mwakamele, Titus Aron, Cathbert Mbilingi na Winniwa Kassala.

Moshi alidai kuwa washtakiwa hao wakiwa na nia ovu walitoa taarifa za uongo mtandaoni na kufanikiwa kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Alidai kuwa washtakiwa hao maarufu kama 'Halo halo' walitoa taarifa za uongo wakitumia ujumbe usemao "Nitumie hiyo hela kwenye namba hii".

Alidai kuwa walikamatwa kwa nyakati tofauti tofauti Ifakara, mkoani Morogoro kwa kosa la kula njama na kutuma jumbe za kitapeli kwa nia ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutoa taarifa za uongo mitandaoni.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa hao wamekuwa wakiwatumia wananchi mbalimbali jumbe za simu za kitapeli pamoja na kupiga simu, huku wakidai wao ni wafanyakazi wa kampuni ya simu na kuwatapeli fedha zao.

Baada ya washtakiwa hao kusomewa mashtaka yanayowakabili walikiri kutenda makosa hayo ndipo Hakimu Maguta alipotoa adhabu hiyo dhidi yao.

Washtakiwa watano ambao ni Fredrick Kanepela, Julius Mwabula, Amiry Luwiso, Tareeq Sadrudin na Ashraf Awadhi waliridhia kulipa faini ya Sh. milioni sita kwa kila mmoja.

Washtakiwa wengine sita akiwamo Frank Kifyoga, Samson Tandike, Michael Haule, Mussa Maganga, Helman Lwambano na Kelvin Mkapila, walipewa adhabu ya kifungo cha miaka mitatu jela kila mmoja baada ya kushindwa kulipa faini hiyo.

Hata hivyo, shauri hilo bado linaendelea mahakamani kwa washtakiwa wengine 13 waliosalia ambao hawakukiri makosa yao.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Madereva, mashabiki wawe makini sana wakati wa safari

**JUZI** kuelekea michezo ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya robo fainali kumetokea matukio mawili ya ajali ya magari ambayo mashabiki wa soka wa klabu ya Simba walikuwa wakiyatumia kutoka Mbeya na Dodoma kuja Dar es Salaam kushuhudia mchezo wa timu yao dhidi ya Al Ahly ya Misri.

Mchezo huo ulichezwa jana kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na mashabiki wengi wa soka.

Hakuna ubishi kuwa timu za Simba na Yanga zina ushawishi mkubwa kwenye soka la Tanzania na zina mashabiki wengi wa soka ndani ya nchi na ukanda wa Afrika mashariki na Kati.

Kutokana na ukubwa wa timu hizi mbili, mashabiki wengi huwa wanasafiri kutoka mbali kuja Dar es Salaam kushuhudia timu zao zikicheza.

Kwa bahati mbaya juzi magari mawili aina coaster yaliyokuwa yamebeba mashabiki wa Simba kutoka Mbeya na Dodoma yalipata ajali na kupelekea majeruhi na shabiki mmoja kupoteza maisha.

Nipashe inatoa pole kwa ndugu na jamaa wa shabiki aliyepoteza maisha na kwa uongozi wa Simba, lakini pia tunatoa pole kwa viongozi wa klabu hiyo.

Pia tunatoa pole kwa majeruhi wote ambao wamepata madhara kwenye ajali hizo za barabarani.

Hata hivyo kuna jambo la msingi la kuwakumbusha mashabiki na madereva wa magari ya abiria wawapo barabarani.

Pamoja na mambo mengine lakini lazima mashabiki kuwa makini na safari zao lakini pia madereva kujitambua na kuendesha magari kwa kwa kufuata sheria na alama za barabarani kuepuka ajali zisizokuwa na ulazima.

Safari za mashabiki zinakuwa na burudani zake kwenye magari na kupelekea kujisahau hata pale madereva wanapoendesha kwa kasi kubwa au kuvunja taratibu za alama za barabarani.

Madereva wa magari haya ya abiria yanayokodiwa na mashabiki hawapaswi kufuata au kusikiliza kile kinachofanywa na mashabiki ndani ya gari kama vile kunywa vileo, kuimba na kucheza muziki.

Wanapaswa kufanya kazi zao kwa weledi kwa kuendesha kwa utaratibu wa sheria za barabarani ili kujikinga na ajali zisizokuwa na ulazima wowote.


Lazima watambue wanapoendesha magari hayo na kuwa na abiria, wanakuwa wamebeba mioyo ya watu ambao wana majukumu huko walikotoka hivyo lazima uendeshaji uwe wa makini wenye kuzingatia sheria zote za barabarani.

Lakini kwa mashabiki ambao ni abiria hawapaswi kufumbia macho vitendo vya madereva wanaovunja sheria za barabarani iwe kwa kuendesha kwa kasi au vinginevyo, ni lazima wawakemee.

Tusikubali kukaa kimya pale tunapoona madereva wanaendesha magari kwa kuvunja sheria za barabarani, tupaze sauti kwa kuwakemea au kuwashtaki kwa askari wa barabarani.

Pamoja na yote, Nipashe tunaungana na wale waliopata majeraha Mungu awasaidie wapone haraka na kurejea kwenye majukumu yao, lakini pole nyingi kwa familia iliyopoteza ndugu yao kwenye ajali hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# TFF ipeleke waangalizi mechi zilizobaki, Ligi ya 'Championship'

Na Adam Fungamwango

**LIGI** ya 'Championship' inayosaka timu zitakazopanda Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao inafikia ukingoni.

Zimebaki raundi nne tu kukamilika ili kuzipata timu mbili za juu zitakazopanda moja kwa moja kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao wa 2024/2025.

Zingine mbili, itakayoshika nafasi ya tatu na ya nne kwenye msimamo zitacheza mechi za mchujo ili kuipata timu moja itakayokwenda kucheza na timu iliyoanguka kutoka Ligi Kuu kwa ajili ya kumalizika nafasi moja iliyobaki ya kucheza ligi.

Msimu huu kumekuwa na mchuano mkali kwenye ligi hiyo tofauti na zile zilizopita.

Timu zimekuwa zikiachana pointi chache huku zikibadilishana nafasi kila baada ya raundi kadhaa.

Kwenye Ligi ya Championship, timu zinazopigania kupanda daraja ni KenGold FC, Pamba FC, Biashara United, Mbeya Kwanza na TMA.

Kwa jinsi pointi zilivyo ni kwamba timu mbili zitakazopanda moja kwa moja zitatokana na hizi hizi, huku zitakazocheza 'play off' zikionekana kabisa kuwepo miongoni mwa timu hizo nne.

Timu inayoonekana kwa kiasi kikubwa inaweza kupanda moja kwa moja ni KenGold ambayo ina pointi 60 na inahitaji pointi sita tu kati ya mechi nne ilizobaki nazo ili msimu ujao icheze Ligi Kuu.

Timu zilizobaki zinasubiri nafasi moja iliyobaki na zitakazosalia zitakwenda kucheza mechi za mchujo.

Kwa bahati mbaya sana timu zinazotaka kupanda Ligi Kuu zinakwenda kucheza na baadhi ya timu ambazo hazina cha kupoteza, hivyo kuna uwezekano mkubwa wa kupanga matokeo.

Nasema hivi kwa sababu imeshatokea huko nyuma kesi za upangaji wa matokeo kwenye mechi za Ligi ya Champioship, huku baadhi ya viongozi wakifungiwa.

Katika soka la Tanzania, Ligi ya Champioship ndiyo ushahidi wa upangaji wa matokeo umeshawahi kupatikana na wahusika kufungiwa, si mara moja wala mbili.

Mfano mdogo tu wiki hii Mbeya Kwanza inayosaka kupanda Ligi Kuu, inacheza na Cosmopolitan iliyo nafasi ya tisa na haihitaji lolote lile, hapa kuna kuwa na tatizo.

Pamba ambayo kwa misimu kadhaa imekuwa ikishia mechi za mchujo inataka msimu huu kupanda moja kwa moja, itacheza dhidi ya Polisi Tanzania timu inayoshika nafasi ya nane, na haina cha kupoteza.

KenGold vinara wa Ligi watacheza na Mbuni iliyo nafasi ya sita huku pointi zake zikiwa mbali na hata kwenda kucheza mchujo.

Mechi kama hizi inabidi ziangaliwe kwa jicho la tatu kwani upangaji wa matokeo unaweza kuwepo, lakini pia idadi kubwa ya mabao inaweza kuonekana.

Wakati Kengold ina pointi 60, Pamba ina pointi 55, huku Biashara United na Mbeya Kwanza zikiwa na pointi 53 kila mmoja, sasa hapa unaweza kukuta hizi zilizofungana pointi zikipata mabao mengi.

Kwa wiki hii naweza kuitetea Biashara United kwani inakwenda kukutana na Transit Camp ambayo ipo nafasi ya 13 na inajikakamua kutaka kubaki Ligi ya Championship, hapa itapata upinzani mkubwa, lakini baada ya mechi hii itakutana na baadhi ya timu ambazo hazihitaji chochote.

Kwa maana hii, TFF inabidi iwe macho na mechi hizo zilizobaki, ichukue tahadhari kwa kupeleka waangalizi ambao watakuwa na kazi moja ya kuangalia mwenendo wa mechi kama kuna viashiria vya rushwa.

Najua TFF wana wataalam ambao kama wakisambazwa kwenye vituo vyote na wasijulikane, wanaweza kurudisha majibu sahihi ya nini kimefanyika.

Klabu nazo inabidi ziwe makini na wachezaji wao kipindi hiki, kwani wanunuzi wa mechi si lazima wainunue timu nzima, wanaweza kufanya hivyo kwa baadhi ya wachezaji tu.

Kuna timu moja ya Champioship ilirekodi mwenendo wa wachezaji wake na mmoja wa viongozi wa timu nyingine waliokuwa na mpango wa kuhujumu timu, na iliwasaidia sana Kamati ya Nidhamu ya TFF kwenye uamuzi.

Tunataka timu zenye uwezo kupanda Ligi Kuu na si kiujanjaujanja, matokeo yake msimu mmoja tu, zinarejea zilipotoka.

HABARI PICHANI

# IBADA YA IJUMAA KUU KATIKA PICHA



Baadhi ya vijana wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, Usharika wa Dodoma Mjini, wakionyesha igizo la jinsi Yesu alivyoteswa kusulubishwa huko Golgota, wakati wa Ibada ya Ijumaa Kuu, kanisani hapo, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akishiriki Ibada ya Ijumaa Kuu katika Parokia ya Mwenyeheri Maria Theresa Ledochowska, Kiwanja cha Ndege, jijini Dodoma jana. **PICHA: OMR**



Vijana wakimsulubisha kijana Andrew Clement, aliyeigiza kama Yesu wakati wa igizo la kumbukizi ya mateso ya Yesu Kristo, wakati wa Ibada ya Ijumaa Kuu katika Kanisa Katoliki Parokia ya Bikira Maria Mpalizwa Mkwawa, mjini Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (kushoto), akitoa salamu zake katika Ibada ya Ijumaa Kuu katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Dodoma Mjini, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Paroko wa Kanisa Katoliki Mugumu, wilayani Serengeti mkoani Mara, Padri Joel Marwa (kulia) na Padri Johnson Kitunze, wakiongoza ibada ya njia ya msalaba katika adhimisho la Ijumaa Kuu, mjini Mugumu, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Waimbaji wa kwaya kuu ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Dodoma mjini, Dayosisi ya Dodoma, wakiimba wakati wa Ibada ya Ijumaa Kuu kanisani hapo, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# BBT kuwezesha vijana 3,000,000 kujiajiri kwenye kilimo

**Na Joseph Mwendapole,**
DODOMA

MRADI wa Jenga Kesho Bora (BBT), unaosimamiwa na Wizara ya Kilimo unatarajia kuwawezesha vijana 3,000,000 kujiajiri kwenye sekta ya kilimo kufikia mwaka 2030.

Hayo yalisemwa jana mkoani hapa na Kaimu Mratibu wa Taifa wa Mradi huo, Michael Nyanga, wakati wa ziara ya wahariri na waandishi wa habari kwenye miradi hiyo iliyoko Dodoma.

Akizungumza katika shamba la pamoja la BBT Chinangali jana, Nyanga alisema programu hiyo inalenga kuwawezesha vijana kuingia kwenye kilimo na kupunguza tatizo la ajira kwa vijana na kutimiza lengo la serikali kufikisha idadi hiyo ya ajira mpaka 2030.

Alisema miongoni mwa malengo ya mradi huo ni kuongeza uzalishaji kwenye kilimo na kuondoa umaskini wa wananchi kwa kuwawezesha kuzalisha kwa wingi mazao ya kilimo na kuwaunganisha kwenye masoko ili wapate faida wanapouza mazao yao.

BBT, alisema inatekelezwa katika miradi minne ambayo ni mashamba makubwa ya pamoja (block farm) na kuna ekari zinazofikia 2,000 kwa sasa nchi nzima na kwamba eneo lingine ni kuwawezesha vijana kupata mitaji.

Alisema kwenye kutoa mitaji kwa vijana Wizara ya Kilimo inashirikiana na taasisi iliyoko chini ya wizara hiyo inayoitwa Agriculture Input Trust Fund ambao unawezesha vijana kupata riba nafuu ya riba ya asilimia 4.5.

Nyanga alisema paka sasa wamewezesha vijana 118 kupata mikopo ya shilingi milioni 950 na kwamba eneo lingine wanalotekeleza mradi wa BBT ni huduma za ugani ambapo wanawawezesha vijana waliomaliza vyuo kwenda kutoa huduma za ugani kwenye maeneo ya wakulima nchini.

"Kwenye eneo la huduma za ugani tumeshaanza na vijana 251 kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ambao tumeshawapeleka kutoa huduma za ugani kwenye mashamba ya pamba na kwa sasa vijana hao wanatoa huduma kwenye wilaya 40 zinazolima pamba nchini," alisema.

Alisema eneo lingine la mradi huo ni kuchimba visima 65,000 wakilenga wakulima wenye ekari 2.5 ambapo wanawekea miundombinu ya umwagiliaji, tenki la maji la lita 5,000 ambapo wanatarajia kuwafikia wakulima 1,40,000 mpaka kufikia mwaka 2030.

Shamba la pamoja Chinangali yenye ekari 1,772, alisema mpaka sasa kuna vijana 261 ambao tayari wameshaanza uzalishaji na tayari wameanza kuzalisha alizeti kwa kulima mashamba ekari 620 kati ya 1,772 wanazolenga kulima eneo hilo.

"Ekari ambazo zinaendelea kusafishwa ukichanganya na hizi 620 ambazo zimeshalimwa tutakuwa tumefikia ekari 1,272 ambazo zimeshasafishwa na lengo la wizara mpaka Mei mwaka huu tuwe tumeshamaliza kusafisha eneo lote la Chinangali ili tuwape vijana amshamba yao," alisema.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji Mitaji ya Umma (PIC), wakitembelea Kituo Kikuu cha Mabasi Msamvu, mkoani Morogoro hivi karibuni. Kituo hicho ni mradi unaoendeshwa kwa ubia Kati ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) unaomiliki 74% na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro 26%. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake watajwa kubeba mzigo mabadiliko tabia nchi

**Na Beatrice Shayo**

WANAWAKE wametajwa kubeba mzigo mkubwa katika mabadiliko ya tabia ya nchi ikiwamo mgogoro wa mazingira na usawa wa kijinsia jambo ambalo linatakiwa kuchukuliwa hatua za ziada.

Daktari Bingwa wa Mionzi katika Hospitali ya AgaKhan, Ahmed Jusaaban, aliyasema hayo jana wakati hospitali hiyo ikiadhimisha Siku ya Wanawake Duniani.

Maadhimisho hayo yamebebwa na kauli mbiu isemayo, "Wekeza katika jinsia ya wanawake kuharakisha maendeleo katika afya ya akili, usawa wa kijinsia na mazingira Tanzania".

Dk. Jusaaban alisema wanawake wanakabiliwa na changamoto za ukatili wa kijinsia, kuongezeka kwa tatizo la afya ya akili, ndoa za ututoni na mabadiliko ya mazingira.

Wanawake kwa ujumla wanabeba mzigo zaidi wa mabadiliko ya mazingira, hivyo maadhimisho haya yanatoa fursa ya kutukumbusha umuhimu wa michango ya wanawake katika sekta ya afya na jamii kwa lengo la kufikia malengo endelevu yaliyowekwa na nchi," alisema.

Jusaban ambaye ni kiongozi wa mradi wa CHOICE, alisema mradi huo unaangalia hasa katika afya, afya ya akili, usawa wa kijinsia na mazingira kwa ujumla.

Alisema Tanzania ni moja ya nchi ambayo imeridhia kushughulikia malengo ya mradi huo kwa kuangalia maendeleo endelevu ya umoja wa Mataifa.

"Tanzania ni moja wapo ya nchi tano ambapo mradi huu wa CHOICE unaangalia maendeleo endelevu ya umoja wa mataifa na Tanzania ni nchi moja wapo ambayo imeridhia kushughulikia hayo malengo," alisema.

Jusaban alisema mradi huo kwa kila nchi unatakiwa kuangalia Tanzania imefikia wapi katika kufikia malengo yake ya kidunia na kujua kama kuna shida zimesababisha kukwamisha malengo endelevu.

Alisema tangu mwaka 2015 malengo ya mradi huo yaliridhiwa na nchi nyingi changamoto kubwa iliyofanya mradi huo kushindwa kuendelea ni kutokana na janga la UVIKO-19 na vita ya Ukraine na Urusi uwapo wa hali mbaya ya kiuchumi katika nchi nyingi.

"Mataifa mengi yalipopitisha malengo endelevu mwaka 2015 yalianza vyema, kwa sababu ya vikwazo kadhaa ikiwa UVIKO-19, vita ya Urusi na Ukraine, nchi nyingi kuwa na hali mbaya kiuchumi, hivyo suluhisho lazima lipatikane ili kuharakisha kufikiwa kwa malengo hayo kabla ya kufikia mwaka 2030," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Huduma ya Afya katika Hospitali ya Aga Khan Tanzania, Sisawo Konteh, alisema Aga Khan inaendelea kuwa thabiti katika kuweka kipaumbele kwa afya ya wanawake kupitia huduma za afya wanazozitoa kwa jamii.

"Kupitia kujitolea kwetu kwa usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake, tumejitolea kushughulikia mahitaji ya kipekee ya afya ya wanawake na kuongeza ufahamu wa masuala ambayo yanawaathiri kwa kiasi kikubwa,"alisema.

Mtaalamu wa Magonjwa ya Wanawake hospitalini hapo, Dk. Muzdalifat Abeid, alisema kuna umuhimu mkubwa wa kujumuisha huduma zote za usaidizi kwa waathirika ndani ya huduma za afya kama vile ushauri na tiba na maeneo salama ya kujihifadhia ili kushughulikia athari za afya ya akili zinazotokana na ukatili wa kijinsia na ubaguzi.

# Wataka mfumo wa taka sifuri usambazwe nchini

**Na Halfani Chusi**

MWENYEKITI wa Ushirika wa Wakusanya Taka Bonyokwa mkoani Dar es Salaam, John Nsyenge, amesema mfumo wanaotumia wa ukusanyaji taka majumbani unaolenga kufikia taka sifuri katika makazi ya wananchi usambazwe maeneo tofauti.

Mfumo huo unajumuisha kutoa elimu kwa wananchi namna ya kutenganisha taka katika makundi manne; taka zinazooza, rejeshi, nyinginezo (zisizo na thamani) na hatarishi.

Aidha, Nsyenge amesema serikali inapaswa kuiga mfumo huo kwa kuusambaza maeneo mengine ili kufikia adhma ya taka sifuri.

Aliyasema hayo jana katika hafla maalumu ya kuzindua makala ya maonyesho ya mfumo wa taka sifuri Tanzania na kusisitiza kuwa, baada ya ukusanyaji wa taka kwa mfumo huo huzigeuza mbolea na kuuza.

"Baada ya kuzikusanya nyingine tunazigeuza mbolea tunauza na tunapata kipato. Tunatengeneza wadudu ambao ni chakula cha kuku na samaki, lakini pia imesaidia kujiajiri.

"Tunapata fedha kutokana na makusanyo ya taka nyumba kwa nyumba" alisema mwenyekiti huyo huku akiiomba serikali kuwaunga mkono.

Ushirika huo unaofadhiliwa na taasisi ya Nipe Fagio umeifanya Bonyokwa kuwa safi na kuwa sehemu ya mfano kwa watu kutoka mikoa mbalimbali kwenda kujifunza namna wanavyofanya kazi.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Bonyokwa, Shabani Maliyatabu, aliusifu mfumo huo akisisitiza ni mzuri kwa kuwa unatenganisha taka katika mafungu manne.

"Kituo kimetoa ajira kwa vijana kwa wa kike na kiume, ni mfumo bora unapaswa kupokewa kwa kila sehemu hapa nchini Bonyokwa yote sasa iko safi," alisifu.

Ofisa Mazingira Jiji la Ilala-Kinyerezi Kanda Namba Nne Piusi Mwalupembe, alisema mfumo huo unafaa na utasaidia kwa asilimia kubwa kufikia adhma ya serikali ya taka sifuri.

"Kupitia mfumo huu kiwango cha taka kinachokwenda dampo ni kidogo sana, taka nyingine zinabadilishwa kwa matumizi mengine. Mfumo huu kama utafanyika katika maeneo yote tutafanikiwa.

"Serikali kwa sasa tunaangalia namna ya kutenga maeneo ya wazi kwa ajili ya kuchakata taka ili kuwawezesha waokota taka kufanya zoezi lao kiurahisi, lakini pia tunaangalia namna ya kupeleka taaluma hii katika maeneo mengine nchini," alisema. Mratibu wa Mradi wa Taka Sifuri Tanzania kutoka Nipe Fagio, Wilyhard Shishikaye, alisema lengo lao ni kuleta mbinu na njia bora zitakazoisaidia serikali kukabiliana na tatizo la taka.



# Samia mgeni rasmi kumbukizi Sokoine

**Na Paul Mabeja,**
DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuwaongoza watanzania kwenye ibada maalum ya kumbukizi ya miaka 40 ya aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania, Edward Moringe Sokoine, itakayofanyika Aprili 12, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Msemaji wa Familia ya Hayati Sokoine, Lembris Kipuyo, alisema ibada hiyo itafanyika katika Kijiji cha Enguik, Monduli Juu mkoani Arusha.

Alisema ibada hiyo ya kumbukumbu ya Hayati Sokoine itahudhuriwa na viongozi mbalimbali wa serikali wakiongozwa na Rais Samia.

Akizungumzia lengo la kuanzishwa kwa Taasisi ya Hayati Edward Moringe Sokoine, alisema ni kuenzi mema aliyoyafanya kwakuwa aliacha alama kubwa ambayo taifa linamkumbuka hadi leo.

Pia alisema Taasisi hiyo imejikita katika masuala ya elimu, kilimo, hifadhi ya mazingira, vyanzo vya maji pamoja na afya.

Kipuyo alisema Hayati Sokoine alifanya mambo makubwa katika taifa la Tanzania ambayo hadi leo yameacha alama kubwa hivyo kupitia siku hiyo Watanzania watapata fursa ya kuelewa kile alichokifanya wakati wa uhai wake.

"Hayati Sokoine alikuwa mzalendo wa kweli, alipenda taifa lake na wananchi wake, alihakikisha kwamba rasilimali za nchi zinatumika na Watanzania wote, aliwatumikia wananchi bila kubagua na alikuwa na hofu ya Mungu katika kufanya kazi zake," alisema.

Pia alisema katika mambo ambayo hayatasahaulika ni pamoja na jitihada zake kwenye kilimo na mifugo, ambapo yeye ndiye alikuwa chachu ya kuanzishwa kwa Chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) ambacho kilianzishwa kwa lengo la kuzalisha wataalam wa kilimo ili kuiwezesha nchi kuwa na uhakika wa chakula.

# Bunge lataka mageuzi elimu VETA

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) imeagiza Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) kufanya mageuzi katika vyuo vyake ili kusaidia taifa kupata wataalam wa kutosha. Makamu Mwenyekiti wa PAC, Japhet Hasunga alisema hayo jana baada ya kutembelea Chuo cha VETA wilayani Ikungi mkoani Singida ambacho kimejengwa kwa zaidi ya Sh. bilioni tatu.

Alisema serikali imejenga vyuo vya VETA ili kupata wataalamu wa kutosha wa kwenda kufanya kazi kwenye viwanda.

"Kule mkoani kwangu (Songwe) kuna kijana wa darasa la saba alitengeneza chopa na anairusha hadi juu lakini changamoto akitaka kuishusha inabidi aizime kwanza ndipo adondoke nayo,sasa VETA ingeweza kumsaidia huyu mbunifu," alisema.

Hasunga alisema kamati ilikwenda mkoani Mwanza na kujionea watanzania walivyounda meli yenye uwezo wa kubeba abiria 1200 na tani 400 za mizigo, hivyo kila kitu kinawezekana kinachohitajika ni dhamira ya kweli ya kuwawezesha na kuwasimamia watanzania.

Mbunge wa Masasi, Geofrey Mwambe, alisema tatizo kubwa vijana hawatengenezwi kubobea katika masuala fulani ya ufundi jambo ambalo wakiingia kwenye soko la ajira wanashindwa.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu ,Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, alisema serikali imedhamiria kutoa ujuzi kwa vijana wa kitanzania kupitia taasisi ya VETA na tayari kuna sekondari chache zimeanza kutoa mafunzo kwa kutumia mitaala ya VETA. "Serikali hivi sasa suala la ujuzi ndio mpango mzima,kuanzia mwaka huu shule 28 za sekondari za serikali na 68 za binafsi zimeanza kutoa mafunzo kwa kutumia mitaala ya VETA ambapo taaluma zinazotolewa zinaendana na upatikanaji wa soko la ajira katika maeneo husika," alisema.

Awali, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa VETA, CPA Anthony Kasore, alisema hivi sasa kuna ujenzi wa vyuo vipya 65 katika wilaya 64 na kimoja cha Mkoa ambavyo vikikamilika vitafanya VETA kuwa na jumla ya vyuo 145 ambavyo vitaongeza udahili wa wanafunzi kuwa zaidi ya 140,000 na hivyo kuongeza uwezo wa wananchi kupata ujuzi katika shughuli mbalimbali za uchumi.

Kasore alisema VETA inaendelea kuimarisha mitaala ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira na kwamba changamoto ya upungufu wa walimu vibali vya ajira vimetolewa na wataajiriwa watumishi zaidi ya 200 kwa ajili ya vyuo 25 ambavyo ujenzi wake umekamilika katika nchi nzima.




Mkuu wa Oparesheni wa Polisi kikosi cha Usalama Barabarani nchini, ACP Nassoro Sisiwaya (kushoto), akisimamia wakati askari akiondoa kibao cha namba kwenye lori T618 BEH ambalo lilikutwa na hitilafu, wakati akiwa katika zoezi la ukaguzi wa vyombo vya moto, mkoani Iringa jana. Kushoto kwake ni Kaimu Mkuu wa Kikosi hicho mkoa wa Iringa, ASP Glory Mtui. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Wanunuzi waliotapeli wakulima mtegoni

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amewaagiza wakuu wa mikoa kushirikiana na halmashauri kuzikamata kampuni zinazodaiwa na wakulima wa tumbaku zaidi ya Sh. Bilioni nne ili kufikishwa mahakamani.

Bashe aliyasema hayo jana wakati wa mkutano wa wadau wa tasnia ya tumbaku uliofanyika jijini hapa.

Alisema ni kosa kubwa sana kukaa na malipo ya wakulima ndani ya mwaka mzima hali inayorudisha nyuma kilimo cha zao hilo.

"Nataka kama hao watu wamekamatwa na kuchukuliwa hatua ili kulipa madeni ya wakulima, nawaagiza wakuu wa mikoa hakikisheni kampuni hizi zinakamatwa na kufikishwa mahakamani ziwalipe wakulima," alisema Bashe.

Mbali na hilo, alimuagiza Mrajisi wa vyama vya ushirika kuhakikisha vyama vinalipa katika mabenki wanayodaiwa ili benki ziendelee kuwawezesha wakulima.

Bashe alisema hadi kufikia Jumatano vyama hivyo viwe vimekutana na kutoka taarifa sahihi kuhusu madai yao kwenye benki.

"Naamini wakulima wamelipa fedha hizi isipokuwa vyama ndivyo vinachelewesha malipo haya, kitendo hiko sio kizuri kwa sababu wanachelewesha maendeleo ya wakulima," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Tumbaku Tanzania, Stanley Mnozya, alisema wakulima wanadai fedha kutoka kwenye kampuni na madai hayo yamekuwa ya muda mrefu.

Alisema lengo lao ni kuona wakulima wanapata stahiki zao ambazo zitawasaidia kupiga hatua katika kilimo ambacho wanafanya.

Hata hivyo, alisema msimu ujao wamejipanga kuzalisha kwa wingi zao hilo ili kuingia katika ushindani wa uzalishaji zao hilo.

Alisema Zimbabwe unaongozwa kwenye uzalishaji lakini wanajipanga kuhakikisha wanawafikia na kuwapita katika uzalishaji wanaofanya.

Mmoja wa wakulima, Hamza Rajabu, aliomba serikali kuingilia kati madai yao ili kulipwa stahiki zao wanazodai kutoka kwa kampuni zilizochukua tumbaku.





## Wakiukaji sheria wawekwa mtegoni

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani (ZARTS), Ali Haji Zubeir, amesema atawachukulia hatua za kisheria madereva wanaokwenda kinyume cha sheria.

Zubeir aliyasema hayo jana alipozungumza na wadau wanaosafirisha abiria kutoka mjini kwenda nje ya mji, hafla iliyofanyika katika ofisi za mamlaka hiyo, Mwanakwerekwe, Unguja.

Alisema kuna ongezeko la tabia kwa baadhi ya madereva wa gari za abiria kuvunja taratibu za sheria za barabarani jambo ambalo halipaswi kuachiliwa kuendelea.

Zubeir alitoa kauli hiyo kutokana na malalamiko yaliyotolewa na madereva wanaosafirisha abiria kwa magari ya Nungwi kuwepo madereva wanaochukua wafanyakazi wa hoteli kuchukua abiria.

Alisema kasi ya uvunjifu wa sheria za barabarani imefikia hatua ya kuwa tishio, hivyo mamlaka inakusudia kuchukua hatua ya kuwafutia leseni madereva ambao watathibitika kuvunja sheria na taratibu hizo.

Mkurugenzi huyo pia amekemea tabia ya baadhi ya madereva wa magari ya Nungwi kutangaza kituo cha kwanza cha kushusha abiria kuwa ni Mahonda kinyume cha mkataba wa leseni walizoomba kufanya biashara.

Aidha, Zubeir aliwataka madereva wanaochukua abiria kufuata sheria kwa kuacha kutangaza bei za nauli wanazozitaka wenyewe hasa katika kipindi hiki cha mwezi mtukufu wa Ramadhani.

"Tumepata taarifa kuwa wapo madereva wanaotangaza bei zao kinyume na bei elekezi zilizotolewa na mamlaka husika na kusababisha malalamiko kwa abiria ya kutozwa nauli kinyume na sheria", alisema.

Madereva wa magari ya abiria waliomba mamlaka kuwafuatilia madereva wanaochukua wafanyakazi wa hoteli kwa sababu wanakiuka kulipa ushuru kwa kuchukua abiria kinyume cha mikataba ya maombi ya biashara.

## SMZ yajinasibu kuwekeza kwa vijana kwa maendeleo ya uchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Shariff Ali Shariff, amesema vijana ndio tegemeo la kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii, hivyo serikali itaendelea kuthamini mchango unaotolewa na serikali ya Marekani kupitia programu za Shirika la Misaada Kimataifa la Marekani (USAID) kusaidia vijana.

Aliyasema hayo jana visiwani hapa wakati akizungumza baada ya uzinduzi wa mpango wa kuwawezesha vijana kupitia mradi wa Feed the Future Imarisha Sekta Binafsi Tanzania. Alisema kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, asilimia 37 watu walioko Zanzibar ni vijana wenye umri kati ya miaka 25 na 35, hivyo kuna haja ya serikali kushirikiana na washirika wa maendeleo kuwekeza kwa vijana kwa kuwapangia mipango madhubuti ya uwezeshaji.

Mataifa mengi, alisema yaliyoendelea huwekeza kwa vijana kwa kuwajengea uwezo katika nyanja mbalimbali na kuwapatia rasilimali za kujiendeleza. Pia alisema mpango huo umekuja wakati mwafaka na pamoja na mambo mengine, utasaidia kutatua changamoto zinazowakabili vijana zikiwamo ukosefu wa mitaji, taaluma ndogo, teknolojia hafifu, kukosekana ubora wa bidhaa wanazozalisha na kufikia fursa za masoko ya ndani na nje.

Waziri huyo alisema serikali inachukua jitihada mbalimbali ikiwamo kuweka mipango na sera zinazotekelezeka ambazo huelekeza mikakati ya kuwaendeleza vijana kupitia sekta ya umam na binafsi.

Aliitaja mipango hiyo ni kuwapatia mikopo isiyo na riba, kusaidia programu za mafunzo, mafunzo kazi, kuwaunganisha na kazi nje na ndani ya nchi.

"Pamoja na jitihada hizo, serikali imejizatiti kuendelea kuwekeza kwa vijana kwa kuhakikisha wanasaidiwa kujikita katika shughuli za kiuchumi kama vile ujasiriamali, kilimo, uchumi wa kidigital na uchumi wa buluu," alisema.

Mkurugenzi Mkazi wa USAID Tanzania , Craig Hart, alisema Marekani inajivunia kushiriki katika kufanya tathmini ya mahitaji ya kifedha kwa vijana na kuonesha njia ya kuwasaidia kufikia ndoto zao.

Alisema kuwa mpango huo unaofadhiliwa na shirika hilo kupitia mradi wa Feed the Future Tanzania Imarisha Sekta Binafsi, utawaongoza vijana katika hatua zinazohitajika kupata vyanzo vya fedha na kuimarisha shughuli zao Tanzania Bara na Zanzibar.

Mradi huo, alisema utawaunganisha wafanyabiashara 3,000 kAtika mnyororo wa thamani wa kilimo katika miaka mitatu ijayo na USAID inatoa ruzuku mpya tano kwa Jumuiya ya Kitaifa ya Wafanyabiashara Zanzibar (ZNCC), Kitovu cha Ubunifu cha Cube Zanzibar, Agriedo, Muungano wa Wazalishaji Kilimo wa Ukanda wa Kusini (SCAAP) na Uwezeshaji wa jumuiya Zilizotengwa (E-MAC Tanzania).



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki ya KCB Tanzania, Balozi John Ulanga (kulia), akizungumza na Mwenyekiti wa Bodi ya Shariah ya KCB Sahl Banking, Shekhe Khamis Mataka wakati wa hafla ya futari na wateja wake iliyoandaliwa na benki hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Tume yasisitiza elimu vyombo vya ulinzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, imesema vyombo vya ulinzi na usalama vinahitaji elimu katika matumizi ya sheria wakati wa utekelezaji wa majukumu kwa sababu kuna viashiria vya kutumia mabavu.

Akizungumza na waandishi wa habari visiwani hapa jana wakati akitoa taarifa ya uchunguzi maalum uliofanywa na tume hiyo kati ya Machi na Mei, 2022 na Machi hadi Juni, mwaka jana, Kamishina wa Tume hiyo, Khatib Mwinyi Chande, alisema malalamiko 71 kati ya 90 yaliyoshughulikwia Zanzibar ni ya uvunjifu wa haki za binadamu na 19 yalihusisha ukiukwaji wa misingi ya utawala bora.

Bila kuzingatia sheria wakati wa utendaji kazi, alisema kunasababisha ukiukwaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora. Kwa mantiki hiyo, alisema ni vyema vyombo hivyo vikapewa elimu jinsi ya kuheshimu na kulinda haki za binadamu na utawala bora.

Mwinyi alisema tume hiyo ilikamilisha na kuhitimisha uchunguzi wa malalamiko 11 wakati malalamiko 66 uchunguzi wake unaendelea.

Alisema katika kipindi cha Machi hadi Mei, 2022 tume ilifanya uchunguzi maalum mmoja na Machi hadi Juni, 2023, ilifanya uchunguzi mara mbili kwa kwa njia ya mahojiano na wahusika walioguswa kwenye malalamiko na uchunguzi sambamba na kufika kwenye maeneo ya matukio ili kupata ukweli wa malalamiko hayo.

Kuhusu uchunguzi wa kifo cha mahabusu Amina Adam Said ulifanyika baada ya taarifa kwamba alikamatwa kwa tuhuma za kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kuwapo kwa utata kwa aliyesababisha kifo chake kati ya maafisa wa kitengo cha mji salama na askati wa polisi kituo cha Madema.

Alisema uchunguzi umebaini Amina akiwa na wenzake wawili, walishikiliwa kwa saa kadhaa na askari wa kitengo cha mji salama kabla ya kufikishwa kituo cha polisi Madema.

Katika uchunguzi huo, alisema ilionekana maafisa wa kitengo hicho waliwashikilia kwa muda huo wakiwalazimisha kurejesha fedha kwa kuwataka jamaa zao mbalimbali kuwatumia fedha kwa njia ya simu vitendo ambavyo ni kinyume cha sheria na mazingira yanaonesha urejeshaji wa fedha hizo Ulifanyika kwa kutumia nguvu ikiwAmo kuwapiga.


Kamishna huyo alisema kifo cha Amina kilitokana na sababu isiyojulikana kwa kuwa uchunguzi uliofanyika ni wa nje ya mwili wa marehemu ambao hauwezi kutoa sababu ya moja kwa moja ya chanzo cha kifo.

Hata hivyo, alisema ushahidi wa mazingira uliopatikana wakati wa uchunguzi ulionyesha kuwa Amina na watuhumiwa wenzake walifanyiwa vitendo cya kikatili ikiwa pamoja na kupigwa na kutishiwa ili kuwalazimisha kurejesha feha walizodaiwa kutapeli.

Alisema baada ya taarifa ya kifo chake, Jeshi la Poisi lilifungua jalada ya uchunguzi na ulipokamilika lilipelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashitaka na iliundwa kamati ya pamoja ya wajumbe kutoka Idara Maalum za SMZ na Jeshi la Polisi kuchunguza jambo hilo na hadi tume inakamilisha uchunguzi, ripoti hiyo haikukamilika.

Kamishna Mwinyi alitoa mapendekezo kwa Jeshi la Polisi kuhakikisha linaimarisha ushirikiano na mamlaka nyengine za usimamizi wa kisheria ili kusaidiana katika kulinda wananchi na mali zao.

Mapendekezo mengine, alisema ni lazima Jeshi la Polisi liwatake wakuu wa vituo vya polisi na maofisa wa jeshi hilo kuzingatia sheria na kanuni kuhusu ukamataji na kuwashikilia watuhumiwa katika vituo ikiwamo ukaguzi wa afya za mahabusu na makabidhiano ya mahabusu hao.



ETI GIGY NAYE ATAOLEWA?
Ukurasa 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI MACHI 30, 2024



# KULIKONI ZUCHU

MASHABIKI wa mwanamuziki wa kizazi kipya kutoka lebo ya WCB, Zuchu, wamekuwa katika hali ya mshangao baada ya msanii huyo kufuta picha zote katika ukurasa wake wa Istagram.

Hata hivyo kwenye ukurasa huo unaofahamika kama "Officialzuchu' amebakisha video moja pekee ya wimbo wake maarufu unaofahamika kama Sukari.

Video hiyo ilioambatana na ujumbe wa Zuchu akiwashukuru mashabiki zake kwa kumuunga mkono na kusababisha ngoma hiyo kufikisha watazamaji milioni 100 kupitia mtandao wa You Tube.

Hata hivyo, maadhi ya watu wameonekana kuwa katika hali ya sintofahamu, wakihoji kwa nini mwanamuziki huyo amechukua hatua hiyo.

Saidi Juma, amesema hatua aliyochukua Zuchu ya kufuta posti zake katika mtandao huo inaleta mashaka kutokana na hali anayoipitia kwa sasa kwa kuwa na maelewano madogo na mpenzi wake Diamond Platnumz.

"Hatujaelewa ni kwanini amefuta vitu vyake muhimu katika ukurasa wake, sijui anataka kutueleza nini? Labda kuna mambo anayoyapitia yamemfanya kuchukua hatua hii," amesema.

Amesema kimsingi wasanii wengi wanapopitia katika matatizo ambayo kwake anayaona magumu, huwa na maamuzi ya kujiondoa au kufuta vitu katika mitandao ya kijamii ili kujiweka katika hali ya utulivu.

"Hatua kama hii wamechukua wasanii wengi maarufu pale wanapopitia mazingira magumu. Pengine yupo kwenye mapito yanayomuumiza kichwa na kuamua kujitenga," amesisitiza Juma.

Miezi michache iliyopita Zuchu alitangaza kuachana na Diamond Platnumz na kila mmoja kuandika kwenye ukurasa wake kuwa yupo singo, na baadae waliondoa tofauti zao na kurudiana tena.

BASI SAWA

## Eti Gigy naye ataolewa?



MWANAMUZIKI mtata wa Bongo Fleva, Gigy Money, amesema kwa sasa anajiandaa kufunga ndoa na mwanaume kutoka Hispania, hivyo ameamua kukaa mbali na maneno ya watu.

Amesema anapotakiwa kuzungumzia wapenzi wake wa zamani, anaweza kuropoka maneno ambayo yanaweza kumuharibia na ndoa yake ikayeyuka.

"Msitake kuniharibia ndoa, nataka kuolewa na mwanaume wa Hispania, hivyo nakuwa makini kuongea naweza kusema maneno kila kitu kitaharibika," amesema.

## Harmonize kalitibua kwa Mandonga

BONDIA mwenye vituko vingi, Karim Mandonga, amesisitiza kwamba mwanamuziki maarufu wa Bongo Fleva, Harmonize, hana uthubutu wa kumrushia ngumi kwani yuko sawa na mtoto.

Amesema tangu alipoomba apangiwe pambano, yeye Mandonga ameshajitoa na kamwe hataitaji pesa kupigana naye.

"Siwezi kuchukua hata senti moja nikipigana na Harmonize, siwezi kutoza pambano ambalo napigana na mtoto, ninachosisitiza nipo tayari kuandaa pambano naye," amesema Mandonga.





## Mimi Mars yuko sawa

MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, ambaye hivi karibuni aliripotiwa kuwa ni mgonjwa, Mimi Mars, hatimaye ametoa ujumbe mzito kwa mashabiki wake, akiwataka wazidi kumuombea azidi kupata nafuu.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, Mimi Mars , amesema afya yake inazidi kuimarika kila siku na anamshukuru Mungu kumpatia uponyaji ambao kwa sasa anaweza kufanya baadhi ya shughuli zake.

"Leo nimeamua nitume meseji hii kwenu muone kwamba Mimi Mars yupo anazidi kupona na anazidi kufanya bora zaidi, lakini kikubwa zaidi nawashukuru sana kwa maombi yenu na kuniombea katika kipindi hiki ambacho nimekuwa nikipitia matibabu na pia kupona taratibu. Hii inaonesha kwamba ninarudi vizuri kabisa na niko tayari kuanza kazi, tukae karibu na kurasa yangu ili tuweze kuona mambo mazuri," ameandika Mimi Mars.

## Mungu nisitiri mja wako

**Na Adam Fungamwango**

Ni mipango ya Mwenyezi Mungu tu. Kwenye maisha binadamu anaweza kuwa amepitia katika mazingira magumu, mabovu na hata ambayo ni mabaya kwenye jamii, lakini baadaye yakamfikisha kwenye neema, au mafanikio.

Na baada ya hapo kwa binadamu inabaki ni stori na kumbukumbu kwenye maisha yake, lakini akiwa hawezi tena kufanya vile kwa sababu ilikuwa ni mapitio tu, na kwa kiasi kikubwa ni mipango ya Mungu kumfikisha pale alipo.

Ifuatilie kwa makini filamu ya 'Mungu Nisitiri' inayoonyesha jinsi baadhi ya binadamu wanavyopita kwenye mitihani migumu.

Imechezwa na mastaa wengi tu, kina Bi. Hindu, Hemed Suleiman, Baba Haji, Asha Bui, Asia Datchi, Shamira Ndwangira, maarufu kama Bi. Staa na wengineo.

Aisha Bui aliyecheza kama mama Salha, alikuwa amekaa mlangoni mwa nyumba yake. Mara binti yake pekee mdogo akarejea kutoka shule. Akamweleza kuwa anadaiwa fedha za chakula, maji na ulinzi shuleni. Mama akaanza kutoka machozi, mtoto asijue kwa nini mama yake analia.

Aisha anakwenda kwa wifi zake, Bi Hindu na Bi. Staa kuomba msaada wa kumsaidia na mtoto wake, lakini wanamtimua.

Akiwa hajui hili wala lile Salha, anakwenda kucheza na wenzake, lakini manyanyaso anayoyapata kwa kupigwa mara kwa mara, huku akisimangwa kuwa hana baba wala mtu wa kumtetea, linamfanya Salha kumuuliza mama yake alipo baba yake. Hatimaye mama anaamua kumueleza ukweli.

Akaambiwa mama yake aliachana na baba yake akiwa bado hajazaliwa, mama yake akiwa mjamzito. Akaambiwa mama yake alimkimbia mume kutokana na kipigo.

Hali ikawa ngumu kwa Aisha. Alikaa peke yake, lakini hali ikawa ngumu akaenda kwa wifi zake, ambao hawakuwa msaada kwake, kwani nao walikataa kuwa mimba si ya kaka yao, hivyo akawa anahangaika. Baadhi ya majirani walimpa hifadhi hapo alipojifungua mtoto akamwita Salha. Akaanza kufanya biashara ndogo ndogo ili kumudu kumtunza mtoto wake, lakini hali iliendelea kuwa ngumu. Hapo ndipo Salha alipogundua kuwa baba yake alimkimbia. Akaendeleza maisha na mama yake.

Maisha yaliendelea kuwa magumu kiasi cha mama kuamua kujiingiza sasa kwenye biashara ya ukahaba.

Siku moja alipata mteja ambaye alimlipa pesa nyingi zaidi kuliko kawaida. Lakini jamaa huyo akamwambia kuwa yeye alihitaji kumuoa ili aachane na biashara hiyo na kuwa mke mwema na mwanamke anayejiheshimu.

Aisha akamwambia anafanya kazi ile kutokana na ugumu wa maisha na si vinginevyo.

Mtu yule ni Baba Haji ambaye alifunga ndoa na Aisha, wakaishi raha mustarehe na mtoto wao Salha ambaye sasa alifurahi kumpata baba mwingine.





## Abson Nyegela asema kwake 'Haikuwa Rahisi'

Mwimbaji wa muziki wa Injili kutoka mkoani Njombe, Abson Nyegela, amesema mafanikio aliyoyapata kupitia wimbo wake mpya, 'Haikuwa Rahisi' yanatokana na mapenzi ya Mungu.

Akizungumza na BT, Nyegela, amesema wimbo huo uliotengenezwa chini ya studio za EAGLE MJ na video iliyoongozwa Dir Sniger, ni sawa na jukwaa kubwa lililomfanya kuongea na watu wengi kuhusu uponyaji.


"Wimbo huu huu nashukuru mpaka sasa hivi tumepata shuhuda nyingi kutoka maeneo mbalimbali nje na ndani ya Njombe, watu wameguswa sababu ni wimbo uliojaa nguvu za Mungu,"amesema.

Wimbo huo unapatikana kupitia akaunti ya YouTube ya msanii huyo na majukwaa yote ya kusikiliza muziki ya kidijitali.




## Bongo Movie wamebadilika bwana

**Na Adam Fungamwango**



UKIANGALIA filamu nyingi za kisasa na Kitanzania, utagundua kuwa wasanii wetu wamebadika.

Hata kama hawapo vizuri kwenye teknolojia kama wenzetu, Wahispania, Waturuki, Wahindi, Wachina, lakini wamepiga hatua kiasi kwamba filamu za Kibongo zimeanza tena kupendwa na mashabiki kama zamani, miaka ile ya 2010 ambayo ilitikisa.

Hata miaka ile bado kulikuwa na 'ushamba' fulani, na ndiyo maana mashabiki walichukulia poa tu, lakini kadri miaka ilivyozidi kusonga mbele na watu kupata walau uelewa na filamu, hasa baada ya kuingia filamu na tamthilia za kigeni.

Kwa sasa ndiyo tunagundua kuwa kumbe tulikuwa tunaonyeshwa jini kabla ya kuvuka barabara linaanza kuangalia huku na huku.

Jambazi anavua viatu ili kwenda kumuua mtu ndani, mhusika anasafiri kwenda masomoni Ulaya, lakini anaporejea anaonekana na nguo ile ile aliyoenda nayo miaka 10 iliyopita, hata muonekano.

Msichana alikuwa anaigiza anaishi kijijini, lakini muonekano wa nguo, mpaka mitindo ya mnyele ni ile ile ya kisasa wakati mwingine kushinda hata anayekaa mjini wa kipato cha kawaida.

Filamu za zamani zilizowachosha watu zilikuwa na mwelekeo wa maudhui yanayofanana.

Ni lazima kijana masikini awe ametoka kijijini kwenda mjini ambako anapata tabu kwa muda kabla ya kumpata msichana wa kitajiri.

Pia iliwashangaza wengi kuona filamu za vijana matajiri kwenye umri kati ya miaka 25 mpaka 30, ambapo kwa hali ya kawaida si rahisi kuwapata.

Kwenye miaka ya katikati, wasanii walionekana kulalamika na kuitaka serikali kupiga marufuku au kutoka kodi kubwa filamu kutoka nje kwa madai kuwa zinaua soko lao.

Kumbe tatizo halikuwa hilo. Sasa hivi nadhani wamegundua, wamebadilika na mashabiki wameanza kurudia tena kupenda filamu zao. Hivi ni baadhi ya vitu walivyobadika. Filamu kama 'Zahanati ya Kijiji' au 'Saluni ya Mama Kimbo' zinaakisi nilichokiandika.

### SEHEMU ZENYE UHALISIA

Kwa sasa wanaigiza sehemu zenye uhalisia, ambazo watu wengi wanunuzi wa filamu wanaishi, kama Tandale, Mwananyamala, Mbagala, Kigogo, tofauti na zamani ambapo walikuwa wanapenda sana kuigizia 'uzunguni' kwenye majumba ya kitajiri.

Hii imewafanya kuwa karibu na wateja wao, kwa sababu wanayaona maeneo ambao wanayoyafahamu, yaani mashabiki wanaona maeneo yao halisi ya uswahilini.

### MAVAZI, MUONEKANO WA KAWAIDA

Ukizitazama filamu nyingi za sasa utakuta wanaume na wanawake wanavaa zile zile nguo ambazo wanavaa vijana, wazee, au kinadada mitaani. Labda tu eneo ambalo linatakiwa nguo zibadilike.

Kinadada wanavaa madela kama wale wa uswahilini, hii imesababisha mashabiki wengi kuzipenda kwa sababu ni kitu ambacho wanakiona na kukutana nacho katika mazingora yao ya kila siku.

Ni tofauti na zamani ambapo wasanii wengi walikuwa wakivaa kama wanamitindo hata sehemu ambazo hazihitaji hivyo.

### VISA VYA KISWAZI

Visa au maudhui ya filamu nyingi za sasa ni vile ambavyo vinatokea uswahilini na wala si vya kufikirika kama zamani.

Mambo ya kusutana, vigoma, vikoba, umbea, urafiki wa kimakundi, mfarakano kwenye mapenzi, dhana na fikra za ushirikina na vingi vinavyofanana na hivyo, ndivyo vitu vinavyotokea uswazi na kwa hilo wamepiga bao.

### UONGEAJI WA KISWAHILI

Uzungu pia umepungua sana kwenye filamu zetu sasa, ambapo hata wahusika wamekuwa wakiongeza zaidi kiswahili, tena kile cha uswazi kabisa.

Zamani kila muigizaji alikuwa anajitahidi kuogea kwa swaga fulani aonekane ama msomi, au yeye ni mtoto wa uswahilini.

### NGUO ZENYE MAADILI

Tulikuwa tunaona huko nyuma, wasanii wengi wakivaa nguo fupi sana. Hata uigizaji ulionekana kukazania sana maeneo ambayo hayana maadili. Siku hizi waongozaji wanaangalia sana maudhui kuliko kuacha muda mrefu eneo ambalo lina ukakasi kutazama.




# 50 Cent, P Diddy wameumana

UGOMVI wa marapa wakongwe nchini Marekani, 50 Cent na P Diddy, umechukua sura nyingine baada ya kugundulika chanzo cha wawili hao kutoleana maneno makali ni wivu wa kimapenzi.

Sakata zima lilianza baada 50 cent kutoa kumtupia maneno ya kukejeli P Diddy, akionekana kufurahishwa na kufurahishwa kwa kitendo cha msanii huyo kukabiliwa na mashtaka ya unyanyasaji wa kingoni kwa wanawake.

Kinachoonekana furaha baada ya mahakama kumuamuru P Diddy kumlipa mshahara wa kila mwezi, mwanamke ambaye ni mama motto wa 50 Cent aitwae Daphne kwa ajili ya kutoa huduma za ngono.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na kuonekana klatika nyaraka za kesi ya mashtaka yaliyofunguliwa na aliyekuwa prodyuza P Diddy, Rodney Jones akidai kuwa mwanamke huyo ambaye alikuwa mfanyakazi wake Diddy alikuwa akitoa huduma hizo.



## Burna Boy awatolea povu

MWIMBAJI wa Nigeria Burna Boy, amewaita waandishi wa Marekani kama vimelea kutokana na upotoshaji wanaoueneza kwamba amenyoa ndevu zake ili kuwa na mwonekano mpya.

Akiwa mwenye hasira, Burna Boy, amesema kupitia Instagram kwamba picha inayosambazwa na watu hao ilikuwa ya mwaka 2021, na hafahamu kwa nini watu hao wanazusha mambo ya uongo.

"Blogu nyingine za ajabu sana, habari zenu za kila siku zinapotosha eti nimenyoa ndevu. Hii picha nilinyoa ndevu zangu 2021 sio sasa. Hawa vimelea wanaleta mambo ya kijinga," amesema kwa hasira.

## Rebel alivyowakwepa wakware

MWIGIZAJI maarufu kutoka nchini Australia, Rebel Wilson, amesema wasichana wanaokua wajifunze kwake kwa ujasiri, kwani yeye alikaa katika hali ya ubikira kwa miaka 35.

Katika kitabu chake kinachoitwa 'Rebel Rising', ambacho kitatolewa kwa mara ya kwanza Aprili 2, mwaka huu Wilson amefichua kwamba hakupoteza ubikira wake hadi alipokuwa na umri huo, licha ya kupata vishawishi vingi kutoka kwa wanaume.

Amesema amefanya hivyo kwa lengo kuwaonyesha wasichana kwamba hawapaswi kuhisi shinikizo kutoka sehemu yoyote ambalo litapoteza ubikira wao.

"Sio kila mtu lazima apoteze ubikira wake akiwa kijana, watu wanaweza kusubiri hadi wawe tayari au kungoja hadi wawe wamekomaa zaidi," amesema.





## Joeboy hataki wanawake bahili

MWANAMUZIKI wa Nigeria Joeboy, ametangaza kuwa mbali na msichana yeyote ambaye hataki kumtumia pesa na mwenye matumizi mabaya.

Mwimbaji huyo amesema mstari mwekundu utampitia mwanamke ambaye hawezi kupangilia matumizi ya pesa na anakuwa ,mgumu kumsaidia kifedha pale inapohitajika.

" Ningeweka sawa, sio kama ninataka kuchukua pesa zake zote, lakini ninahisi kama ninaweza kukufanyia kitu, na yeye anapaswa. Sio wote wanaosema anaweza kumpa kitu mtu ambaye ana kila kitu," amesema Joeboy.

## Ali baba aumizwa unyanyasaji

MSANII wa uchekjeshaji kutoka Nigeria, Ali Baba, amesema kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa jamii ili kupunguza vitendo vya ubakaji na mauaji.

Akizungumza kwenye kipindi cha Classic FM, Ali Baba alisisitiza utoaji wa elimu hiyo kwa watoto, haswa wale walio chini ya miaka 10 ambao wengi wanakabiliwa na hatari ya vitendo hivyo.

" Mtu fulani aliniuliza siku mbili zilizopita kama unaweza kubadilisha kitu kimoja ulimwenguni kote kingekuwa nini?' Nilimjibu ningetoa elimu rasmi kwa watu kati ya umri wa kuzaliwa na 10 ambao wanakabiliwa na hatari ya unyanyasaji wa kingono na mauaji." Amesema





## Kaya maskini zapewa ruzuku

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MPANGO wa Kunusuru Kaya Maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) umezinasua kwenye ufukara uliopitiliza, kaya 59,904 zilizoko katika Mkoa wa Arusha, baada ya kuzipatia ruzuku ya zaidi ya Sh. bilioni 2.5

Kaya hizo ambazo ni sawa na walengwa 62,667 wa mpango huo walioko katika vijiji na mitaa 577, walipewa ruzuku hiyo ya uhawilishaji fedha katika dirisha la miezi ya Novemba na Desemba mwaka jana.

Mratibu wa TASAF Mkoa wa Arusha, Richard Nkini, alisema mgawanyo wa fedha hizo, umezingatia kaya zilizoko kwenye mpango kwa kila halmashauri.

Mratibu huyo alitaja na kuweka wazi mgawanyo huo kuwa Sh. milioni 551.6 zimegawiwa kwa kaya 13,795 za Halmashuri ya Arusha, Sh. milioni 174.6 kwa kaya 4,385 za Halmashauri ya Jiji la Arusha na Sh. milioni 328.9 kwa kaya 7,761 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu.

Pia alisema Sh. milioni 318 kwa kaya 7,177 katika Halmashauri ya Monduli, Sh. milioni 447.1 kwa kaya 10,111 kwa Halmashauri ya Ngorongoro, Sh. milioni 301.6 kwa kaya 7,769 kwa Halmashauri ya Meru, huku Sh. milioni 388.9 zikigawiwa kwa kaya 8,905 za Halmashauri ya Wilaya ya Longido.

Hata hivyo, alisema lengo la serikali la kuhawilisha fedha hizo ni kuziwezesha kaya hizo,kujiinua kiuchumi na kijamii, kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa na TASAF pamoja mradi wa kuweka akiba kupitia vikundi vya kuweka,kuwekeza na kukopa

Pio alisema TASAF ni mpango wa serikali unaolenga kusaidia kaya masikini nchini,kupitia uhawilishaji fedha moja kwa moja kwa walengwa,ili kuinua hali ya maisha ya kaya zilizoko katika mazingira hatarishi na kuhakikisha kaya hizo, zinatumia fedha kulingana na ruzuku zilizoainishwa za msingi,elimu na afya

"Mpango wa TASAF ni jitihada za serikali za kupunguza umaskini na kukuza maendeleo ya jamii na kupitia programu ya kutoa fedha moja kwa moja kwa walengwa ili kuongeza upatikanaji wa huduma za msingi kama elimu na afya pamoja na kuboresha uwezo wa kaya hizo kujikimu kiuchumi

Hata hivyo programu hiyo imekuwa na matokeo chanya kwa walengwa katika kupunguza umaskini uliokithiri na kuongeza ustawi wa jamii nchini, kupitia tathmini ambayo hufanywa kwa kina na kuhakikisha kuwa misaada inawafikia walengwa kwa usahihi.

# DC aonya waharibifu miundombinu maji

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MKUU wa Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Dk. Suleiman Serera, amewaonya baadhi ya wafugaji wanaokula njama kuharibu miundombinu inayotumika kusambaza maji katika jamii ikiwamo kukata mabomba ya maji, kwa ajili ya kunywesha maji mifugo yao.

Dk. Serera aliyasema hayo jana alipokutana na kuzungumza na wananchi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Orkesumet.

Alilazimika kuwaonya wafugaji hao ili kuunusuru mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira vijijini, unaotekelezwa kwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP).

Pia alisema si jambo la kufurahisha kuona baadhi ya wafugaji wanahusika kuhujumu miundombinu ya maji kwa kukata mabomba kwa kutumia silaha za jadi aina ya sime ili kupata ya kunywesha mifugo maji kwenye maeneo yasiyokuwa rasmi.

"Serikali imetumia fedha nyingi kuwafikishia huduma ya maji mahali mlipo hivyo tunzeni miundombinu ili iwe faida kwenu na kizazi kijacho," alisema Dk.Serera.

Hata hivyo, alisema ameshatoa maelekezo kwa vyombo vya ulinzi na usalama kushirikiana na jamii kuwabaini wahusika ili kuwachukulia hatua kali za kisheria wahusika.

Meneja wa Wakala wa Majisafi na Majitaka Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Simanjiro, Joanes Martin, alisema mradi huo utaboresha upatikanaji wa huduma ya maji kwa wananchi wa eneo hilo.

Vilevile, alisema upatikanaji maji katika Wilaya ya Simanjiro umefikia asilimia 66.7 na mradi huo utakuwa wa ubia kati ya serikali na sekta binafsi.

Ofisa wa RUWASA Makao Makuu, Emmanuel Burton, akizungumzia mradi huo,alisema utawanufaisha wananchi katika mikoa ya Manyara, Lindi, Morogoro, Dodoma na Kagera pamoja na wilaya zingine 15.

Ofisa huyo wa wakala hao, alisema kwa Mkoa wa Manyara, wilaya zitakazonufaika na mradi huo, alizitaja ni Simanjiro, Kiteto na Mbulu.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Zainabu Abdallah (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) wa wilaya hiyo, John Kwagilwa (wa pili kulia), alipotembelea kukagua ujenzi wa mradi wa daraja jipya eneo la Kwamtiga, kata ya Genge juzi, linalotarajiwa kufunguliwa na mbio za Mwenge wa Uhuru Aprili 15 mwaka huu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# NGO zapigwa 'stop' mpango upimaji ardhi

**Tumaini Mafie,** LONGIDO

SERIKALI imeyatahadharisha mashirika ya World Wide Fund (WWF) na Ujamaa Community Resource Team (UCRT), kutoingia katika Wilaya ya Longido mkoani Arusha na mpango wa upimaji wa ardhi yao ili kutekeleza miradi ya uhifadhi jumuishi wa mazingira na kuboresha maisha ya jamii, kwa kuwa kufanya hivyo kutaongeza zaidi migogoro ya ardhi.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Marco Ng'umbi, alionya hayo jana, wakati alipokwenda kuzindua mradi huo, unaolenga kuwanufaisha wafugaji wa jamii ya Kimasai wa Wilaya mbili za Longido na Ngorongoro, kupitia mradi wa uhifadhi shirikishi unaojumuisha binadamu na wanyama.

"Kwa bahati nzuri Wilaya hii ina vijiji 49 na vyote vina ramani na vimepimwa. Hatutegemei UCRT, WWF na wengine kuja kuweka mipaka mipya.

"Mkijaribu kufanya hivyo, ni kutengeneza migogoro ya ardhi.Mnachotakiwa kufanya ni kusaidia kupanga vizuri matumizi sahihi ya kila kipande cha ardhi," alisema.

Mratibu wa UCRT wa Wilaya ya Longido, Jamboi Baramayesu, alisema mradi huo unagharimu dola za Marekani milioni 1.488, sawa na zaidi ya Sh. bilioni tatu.

Kwa mujibu wa Baramayesu, mradi huo unatarajia kuvinufaisha vijiji 10 vya Wilaya za Longido na Ngorongoro.

Zaidia alifafanua, "Mradi huu unahudumia klasta tatu, ambazo ni klasta ya Ziwa Natron na Longido Magharibi, na klasta ya pili ni ya Ziwa Eyasi na Bonde la Yaeda, wakati ya tatu ni Simanjiro na Kiteto.

"Kwa klasta ya Ziwa Natron na Longido Magharibi, vijiji vinavyopitiwa na mradi ni 10, kwa maana ya Ngorongoro vinne na Longido, vijiji sita," alisema.

Richard Mollel, alisema mradi huo ni rafiki kwao, na ni moja ya aina ya mradi unaotakiwa katika jamii ya kifugaji kutokana na kuwa shirikishi na unaojumuisha binadamu na wanyama.

Mkazi mwingine, Hellena John, alisema mradi huo unawapa fursa ya kushiriki katika kuhifadhi vyanzo vya maji, ambavyo vimekuwa vikivamiwa kwa namna moja ama nyingine kutokana na kutokuwepo kwa mipaka thabiti.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Watoto zamani walivyokuwa majasiri wa kuwinda na kukamata wadudu

Na Adam Fungamwango



NI ukweli usiopingika kuwa watoto wa zamani walikuwa watundu mno.

Walikuwa majasiri na walifanya vitu vingi kwa vitendo.

Watoto wa sasa wamekuwa na akili nyingi, ambazo zimechangiwa na kukua kwa teknolojia.

Pamoja na hayo, hawana ujasiri na wanafanya vitu vingi kinadharia zaidi kuliko vitendo.

Wasomaji wengi wameniandikia na kunikumbusha kuhusu tabia ya watoto wa zamani wa mjini na vijijini kuchukua mbwa na kwenda kuwinda.

Walikwenda kuwinda sungura, ndezi na wanyama wengine wadogo, ambapo hata kama ikichukua wiki nzima hawajapata hata mmoja, hawakuacha kazi hiyo. Ilikuwa ni moja tu ya michezo yao na burudani. Wakipata inakuwa sherehe, watachangishana pesa na kupika ubwabwa.

Burudani au michezo mingine ya watoto wa zamani ilikuwa ni kuingia kwenye vichaka kukamata wadudu, kama panzi, balanguru au balale, ambao ulikuwa maarufu sana wakati huo.

Inawezekana mpaka leo bado wapo wanaofanya hivyo, hasa vijijini, lakini kwa kiasi kikubwa mchezo huo umepungua sana. Zamani kuanzia mijini, mikoani mpaka vijijini, ulikuwa ni mchezo maarufu wa watoto wakati huo, hata miji mikubwa kama Dar es Salaam.

Jamaa mmoja akaniambia kuwa zamani wao walikuwa wakikusanyika watoto kuanzia 10 mpaka 15 na kwenda porini, watasaka ndezi au sungura na wakikosa kabisa basi watatafuta kutafuta wadudu waitwao, panzi, balanguru au balale.

Na wanawakamata kwa wingi. Lakini kwa sasa mtoto wake ambaye ana miaka kama ambayo yeye alikuwa anakwenda kuwakamata, anawaogopa.

Hiyo ikanisukuma kuandika makala hii leo.

Mchezo wa watoto kuchukua mbwa na kwenda kuwinda, au kukamata wadudu jamii ya nzige ulikuwa maarufu sana nchini Tanzania

Ulikuwa ikifanywa na watoto kuanzia miaka saba na kuendelea kutegemea mtoto mwenyewe makuzi yake, hadi kuja kuuacha mchezo huo.



Chini ya miaka hiyo walikuwepo, lakini mara nyingi walikuwa wakikatazwa, kwa sababu pia haikuwa rahisi sana kukamata wadudu hao. Ilihitaji utayari, ukakamavu, mbinu, na uvumilivu wa hali ya juu. Na watoto walitembea kwa umbali mrefu.

Haikuwa rahisi hata hivyo kuwapata sungura, ndezi kwa sababu watoto ambao walikuwa wakifanya kazi hiyo wakati wa likizo za shule, waliweza kuwapata mara chache sana.

Hata panzi, barangulu au balale haikuwa rahisi kuwakamata kwa sababu walikuwa wakijilinda na miiba mikali na wajanja sana kuruka na kuepuka hatari. Kukamata balanguru au balale na panzi ulikuwa ni ufahari mkubwa kwa mtoto wa miaka hiyo kwa sababu unaonekana ni jasiri.

Hakuna chochote walichokuwa wakipata watoto. Hawakuwa wakilipwa. Ilikuwa ni michezo tu ya kitoto. Ilikuwa ni kama burudani na walikuwa akijisikia raha sana na michezo ile.

Mwenye kukamata wengi ndiye mwamba, au mjanja kuliko wenzake.

Watoto walitoka majumbani mwao na kutembea kwa umbali mrefu kwa kazi hiyo tu ya kusaka balanguru ambao walikuwa hata hawaliwi.

Hawakujali kutembea kwenye nyasi ndefu, kukatwa na majani yenye miba. Kuchomwa na miiba. Majani ya kuwasha. Kupambana na jua kali. Mvua na vikwazo vingi na hata wakati mwingine kukutana na wanyama wasumbufu.

Na kuna wakati walikuwa wakinyimwa hata chakula nyumbani. Kwao wala haikuwa tatizo. Walichohitaji ni furaha ya moyo wao. Kuwakamata wadudu hao tu. Kwani ni furaha na faraja tosha kuliko chochote. Hata kula.

Jamaa mmoja alinimbia yeye na watoto wenzake wanane miaka ya katikati ya 1980, walitoka kwa miguu kutoka majumbani kwao Buguruni, hadi maeneo ya Jangwani kusaka balale.

Na katika harakati hiyo alipoteza shati. Pamoja na kupata balale wengi, lakini aliporudi nyumbani alitembezewa kichapo kwa kupoteza shati. Na kwa wakati huo ikumbukwe nguo zilikuwa adimu sana kulipata.

Mwingine akaniambia kuna wakati wakitoka mapumziko shuleni wanafanya kazi ya kukamata balanguru na inafika wakati madaftari yanaanguka wao hawana bahari.

"Kweli mkuu huu mchezo tulikuwa tunaupenda sana watoto wa miaka hiyo. Inafikia kipindi madaftari yanaangua huna habari. Sasa ngoja urudi nyumbani. Upambane na kibano. Kwanza umechelewa kurudi shule, pili madaftari yamepungua." Alisema mchangiaji huyo.

Yupo aliyekumbusha kuwa unakwenda kuwakamata balale kwenye nyasi ndefu sana na kuna mabua ya mahindi ambayo yamekauka, hivyo ukipita hovyo yanakata kama kisu. Yanaweka mikwaruzo kwenye ngozi, halafu jioni unakwenda kuoga. "Haki ya Mungu unawashwa utafikiri nini."

Mchangiaji mwingine yeye alikumbushua staili ya kubaka balanguru, akisema kuwa inabidi mkono uukunje kama kibakuli ili umkamate bila matatizo, kwa sababu wadudu hao ni wana miiba mikali ambayo mara nyingi ilikuwa ikiwachoma watoto. Aliyekuwa makini kuvumilia kuchomwa, mjanja, na kwenda umbali mrefu zaidi ndiye aliyewapata wengi zaidi.

"Mkuu watoto tunajipanga kwenye msitu wa majani kama tunakwenda vitani. Kumbe tupo bize kukamata balanguru. Lakini mtindo ule nadhani unasaidia watoto kuwa wakakamavu, wavumilivu, kujituma na kutokata tamaa kwenye maisha." Huyo ni mchangiaji mwingine alisema.

"Nakumbuka tukiwa darasa la kwanza na la pili tulikuwa 'tunawababa' hasa wale wakubwa zaidi kisha tunachimba vishimo vidogo chini tunawaweka na kuwafunika na vioo.

Basi wakianza kutembea tembea humo ndani ya vishimo tunafurahi ile mbaya kuwa tunaangalia sinema. Duh. Jamani zamani ilikuwa raha sana. Leo hii mwanangu akiona panzi mkubwa anapiga mayowe kwa woga." Aliandika mwingine.

**Tuma meseji 0716 350534**

**HABARI KIMATAIFA**

# Russia yapiga kura turufu kuilinda Korea Kaskazini

**NEWYORK,** MAREKANI

RUSSIA imetumia kura ya turufu kupinga kurefushwa kwa muda wa kundi la wataalamu wa Umoja wa Mataifa wanaofuatilia vikwazo vya kimataifa vilivyowekwa dhidi ya Korea Kaskazini.

Tume hiyo inachunguza kama kuna ukiukwaji wowote wa vikwazo hivyo vilivyowekwa kufuatia mipango ya nchi hiyo kutengeneza silaha za nyuklia.

Hatua hiyo imekuja wiki kadhaa baada ya kundi hilo la wataalamu kusema linachunguza ripoti ya ubadilishanaji wa silaha kati ya Russia na Korea Kaskazini.

Uamuzi huo umeibua hisia mseto katika nchi wanachama wa baraza hilo.

Marekani kupitia msemaji wa wizara ya mambo ya nje Mathew Miller, ilisema Russia imetumia kura ya turufu kwa manufaa yake binafsi na juhudi za kuzuia kundi hilo kuchunguza maovu yake na Korea Kaskazini.

Wizara ya Mambo Kigeni ya Korea Kusini, ilieleza Russia ilifanya uamuzi usiofaa licha ya kuwa mwanachama wa kudumu wa Baraza la usalama la Umoja wa Mataifa.

**DW**

# Vikosi vya Israel vyaishambulia nchi ya Syria

**ALEPPO,** SYRIA

WATU 36 wameuawa katika mashambulizi ya anga yaliyofanywa na vikosi vya Israel karibu na mji wa Aleppo nchini Syria, jana.

Wizara ya Ulinzi ya Syria, ilisema kuwa mashambulizi hayo yalitokea maeneo kadhaa katika vijiji vilivyoko Aleppo majira ya saa 1:45 asubuhi.

Shirika la Uangalizi wa Haki za Kibinadamu la Syria (SOHR), lenye makao makuu nchini Uingereza lilisema maeneo yaliyolengwa ni maduka ya silaha yanayotumiwa na kundi la wanamgambo wa Lebanon linaloungwa mkono na Iran Hezbollah.

Israel haijaeleza chochote kuhusu mashambulizi hayo dhidi ya Syria.

Likinukuu vyanzo viwili vya usalama, shirika la habari la Reuters linaripoti kuwa wapiganaji watano wa Hezbollah ni miongoni mwa watu waliofariki na kufanya idadi ya vifo kuwa 38.

Wizara hiyo ilisema raia na wanajeshi wa nchi hiyo pia waliuawa.

Maeneo yanayolengwa ni pamoja na karibu na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Aleppo.

**BBC**

# Rais Senegal azungumza na mshindi wa uchaguzi

**DAKAR,** SENEGAL

RAIS wa Senegal, Macky Sall, amekutana na mshindi wa nafasi hiyo katika uchaguzi mkuu uliofanyika wiki iliyopita Bassirou Diomaye Faye, na kufanya mazungumzo katika ikulu ya nchi hiyo.

Taarifa kutoka Ikulu ya Senegal, ilisema viongozi hao walijadiliana kuhusu masuala muhimu ya serikali pamoja na mipango ya sherehe za kuapishwa. Ushindi wa Faye (44) unatarajiwa kuthibitishwa katika siku chache zijazo na kuchukua rasmi madaraka kabla ya Aprili 2, mwaka huu.

Sall na Faye wamekutana baada ya wiki kadhaa za mzozo kuhusu mchakato wa uchaguzi, jambo linalofanya makabidhiano ya madaraka yawe ya haraka.

Tume huru ya uchaguzi nchini humo, ilitangaza matokeo ya awali ya uchaguzi ambayo yamempa ushindi wa kishindo mgombea wa upinzani Bassirou Diomaye Faye kwa kupata asilimia 54.28 ya kura, huku mgombea kutoka muungano wa vyama tawala, Amadou Ba akiambulia asilimia 35.79.

Ushindi wa mpinzani huyo ambaye alikuwa gerezani siku kumi kabla ya kufanyika uchaguzi, sasa ni lazima uidhinishwe na Baraza la Katiba.

Iwapo ushindi wa Faye utathibitishwa na kuapishwa itakuwa ni mara ya kwanza kwa mgombea wa upinzani kushinda katika duru ya kwanza ya uchaguzi wa rais tangu Senegal ijipatie uhuru wake mwaka 1960.

Sall aliibua mzozo wa kisiasa mwezi Februari baada ya kutangaza kuahirisha uchaguzi wa rais akielezea kuwepo kwa wasiwasi wa usalama katika taifa hilo lenye watu karibu milioni 18.

Hatua hiyo ilizusha maandamano ya umma yaliyosababisha vifo vya watu wanne, kabla ya Mahakama ya Katiba kuamuru uchaguzi huo ufanyike Machi 24.

Rais wa Marekani Joe Biden, amempongeza Faye kwa ushindi aliopata na kutarajiwa kuapishwa kuwa rais wa tano.

**DW**




Majaji wa Mahakama ya Kimataifa ya Sheria wakisikiliza kesi kuhusu athari za kisheria kwa Israel kukalia maeneo ya Wapalestina hivi karibuni. **PICHA: REUTERS**

# Jacob Zuma marufuku kuwania urais

**PRETORIA,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, amezuiwa kugombea nafasi hiyo katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Mei mwaka huu.

Hata hivyo, tume ya uchaguzi nchini humo (IEC), haijatoa maelezo yoyote kuhusu zuwio hilo.

Hata hivyo, hukumu aliyopewa kiongozi huyo 2021 na kufungwa jela kwa makosa ya kudharau mahakama inaonekana ni moja ya kigezo kilichomuondoa kwenye kinyang'anyiro hicho.

Kitendo cha Zuma kuungwa mkono na chama kipya cha Umkhonto we Sizwe (MK), umeonekana kuwa tishio kwa chama tawala cha African National Congress (ANC), ambacho kimemsimamisha uanachama.

Zuma mwenye umri wa miaka 81 alihudumu nafasi ya urais kuanzia 2009 hadi 2018, alipolazimishwa kujiuzulu kwa tuhuma za ufisadi.

Chama kipya cha Zuma kimepewa jina la mrengo wa zamani wa kijeshi wa ANC, na kinamfanya kujiona kama mrithi wa kweli wa mizizi ya mapinduzi ya chama hicho tawala.

ANC iliitaka tume ya uchaguzi ya Afrika Kusini kufuta usajili wa MK, lakini ombi hilo lilikataliwa.

Zuma amekuwa akiongoza kampeni za chama kipya cha MK na lilikuwa jina la kwanza kwenye orodha ya wagombea wao, lakini tume hiyo ilipokea pingamizi dhidi yake kuwa huenda akawa mbunge.

Badala ya kumpigia kura rais moja kwa moja, raia wa Afrika Kusini huchagua wabunge ambao chama chochote kinachopata idadi kubwa ya wawakilishi, kiongozi wa chama hicho anakuwa rais.

"Katika suala la rais wa zamani Zuma, tulipokea pingamizi, ambalo limekubaliwa," alisema mkuu wa tume ya uchaguzi Mosotho Moepya.

Alisema tayari wamekifahamisha chama ambacho kilimteua kuwania nafasi hiyo.

Baada ya uamuzi huo, Zuma ana muda siku tatu kukata rufani.

**BBC**

# JK akunwa kasi ukuaji taasisi za fedha

Na Mwandishi Wetu

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, ameeleza kuridhishwa na kasi ya ukuaji pamoja na uimara wa taasisi za fedha.

Aidha, amezisisitiza kuendelea kujiendesha kwa weledi zaidi ili ziweze kuongeza tija katika kuchochea ongezeko la uwekezaji na ukuaji wa uchumi wa nchi kupitia sekta mbalimbali ikiwamo biashara.

Akizungumza katika hafla fupi ya futari iliyoandaliwa na Benki ya NBC kwa ajili ya wateja wake jijini Dar es Salaam juzi, Kikwete aliitumia benki ya NBC kama mfano muhimu katika kuthibitisha uimara wa taasisi hizo.

Alisema pamoja na kuongeza viwango vya mikopo na huduma mbalimbali kwa wateja pia, zimeweza kutengeneza faida kubwa na hivyo kuendelea kijiimarisha zaidi.

"Ninapotoa pongezi na shukrani ninamaanisha kwa dhati kabisa kwa kuwa mabadiliko mengi ya taasisi ya kifedha yalifanyika mimi nikiwa Waziri wa Fedha kwa wakati ule, hivyo najua vema tulipo sasa na tulipotoka.

"Leo hii nikiona benki zinatangaza faida kwa mabilioni ya fedha zinathibitisha wazi kabisa kuwa zile mabadiliko tuliyofanya kipindi kile yamefanikiwa," alisema na kutolea mfano Benki ya NBC iliyotengeneza faida ya Sh. bilioni 122 kwa mwaka uliopita.

Kikwete alieleza namna wateja walivyopitia wakati mgumu kupata huduma za kifedha kwenye taasisi hizo kabla ya serikali kuingilia kati na kuchukua hatua mbalimbali ikiwamo kufunga na kubadili muundo wa uendeshaji na umiliki kwa baadhi ya benki hizo.

"Leo hii changamoto zote zimebaki historia. Fedha katika uchumi ndio damu ya uchumi. Sekta ya fedha ikitetereka ndio chanzo cha uchumi kuporomoka. Uchumi wa nchi unategemea sekta ya fedha, hivyo ikitetereka kila kitu kinaharibika. Hivyo ninawapongeza sana NBC na taasisi nyingine zote kwa kuendelea kutoa huduma zenu kwa weledi, huku pia mkiendelea kujiimarisha kimitaji," alisema.

Kuhusu matukio ya uandaaji wa futari, Kikwete alisema yanaongeza imani kwa wateja wa benki hiyo kwa kuwa ni moja ya kithibitisho kuwa, uhusiano wa benki na mteja haushii katika biashara pekee, bali pia unagusa imani za wateja.


Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, alisema kilichofanyika ni mwendelezo wa utaratibu wa benki hiyo kwa miaka 15 sasa ikilenga kujumuika na wateja wake kama hatua ya kuonyesha mshikamano na umoja katika kipindi cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhan.

Alisema benki hiyo inaheshimu Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kutokana na ukweli kwamba, ni kipindi ambacho mwanadamu anajiweka karibu na Muumba wake kupitia mfungo na kufanya maombi.

"NBC ndiyo benki ya kwanza kubwa kuanzisha huduma za kibenki zinazofuata misingi ya kisheria kupitia La Riba Banking ikiwamo akaunti za akiba na biashara kwa watu binafsi, wajasiriamali na kampuni makubwa.

"Benki pia inayo akaunti ya muda maalum (fixed deposit) inayofuata misingi ya sharia yaani 'Mudharaba'. Zaidi kupitia dirisha hilo la La Riba tunatoa huduma ya mikopo kwa wafanyanyabiashara wakubwa na wa kati, wajasiriamali wadogo na wafanyakazi wa sekta ya umma na sekta binafsi," alisema.

Hafla hiyo ya futari ilihudhuriwa na wageni mbalimbali wakiwemo viongozi wa serikali, viongozi wa dini wakiongozwa na Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Walid Alhad Omar, viongozi wa vyama vya siasa, wateja, mawakala pamoja na wafanyakazi wa benki hiyo.




Rais mstaafu Dk. Jakaya Mrisho Kikwete akipokea zawadi maalum kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi, wakati wa hafla ya futari iliyoandaliwa na benki hiyo, kwa ajili ya wateja wake, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mama Mariam ahimiza elimu ya hedhi shuleni

Na Mwandishi Wetu, WETE

MKE wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora (ZMBF), Mama Mariam Mwinyi ameitaka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuandaa muongozo wa kutoa elimu ya hedhi salama kwenye shule zote za msingi na sekondari za Unguja na Pemba.

Mama Mariam aliyasema hayo kwenye hafla ya ugawaji wa taulo za kike kwa wanafunzi wa shule mbalimbali za msingi na sekondari Jadida, Wete mkoa wa Kaskazini Pemba, iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na taasisi nyingine za umma na binafsi.

Alisema wanafunzi wamekua wakipitia wakati mgumu kwa kukosa baadhi ya vipindi vya masomo na kuchangia kushuka kwa viwango vya ufaulu.

Mama Mariam alisema suala la hedhi salama limekuwa changamoto kwa kukosekana uelewa sahihi kwa watoto wa kike na jamii hivyo ameitaka Wizara ya Elimu kuweka mikakati madhubuti na kuongeza uelewa kwa jamii.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Zanzibar Leila Mohd Mussa alisema, serikali imekuwa ikichukua juhudi mbalimbali juu ya suala la hedhi salama lakini bado kuna changamoto ya uelewa mdogo kwa jamii hasa kwa baadhi ya wazazi kushindwa kuwaeleza watoto wao njia salama za kujihifadhi wanapokuwa kwenye kipindi hicho.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa ZMBF, Fatma Fungo, alisema ugawaji wa taulo hizo kwa wanafunzi wa kike utawasaidia kupunguza usumbufu wanaopitia wanafunzi wa kike wanapokuwa kwenye mizunguko ya hedhi zao.

Alisema taulo hizo zitawasaidia kuwa kwenye hedhi salama na kuwasaidia kutimiza ndoto zao hasa wanapokuwa katika ada zao za mwezi.

ZMBF, mbali na shughuli nyingi inazofanya ikiwamo kupiga vita udhalilishaji, masuala ya wanawake, vijana na Watoto, pia inaendeleza kampeni yake ya "Mariam Mwinyi Walkathon" ambayo imewagusa wananchi wengi na kuwafuata walipo ili uchunguza afya zao na kufanya matibabu.

Kampeni hiyo ina lengo la kuimarisha afya za wananchi na kutekeleza mikakati ya, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia kampeni ya "Afya Bora, Maisha Bora" inayowafikishia huduma bora za matibabu wananchi wake.

# RC ataka majibu hoja za CAG

Na Gideon Mwakanosya, MBINGA

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, amewaagiza wakuu wa Idara katika Halmashauri kushiriki ipasavyo katika kuandaa majibu ya hoja na utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Kanali Abbas ametoa maagizo hayo kwa nyakati tofauti wakati anazungumza katika kikao cha kujadili utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 katika Halmashauri za Nyasa, Mbinga Mji na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga.

Alitoa maagizo hayo juzi baada ya kutoridhishwa na utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya LAAC kwenye Halmashauri hizo.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Kamati ya Bunge ya LAAC, Agosti 2023, ilitoa maagizo manne ambapo hadi sasa hakuna agizo hata moja lililotekelezwa.

Vilevile, katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, LAAC ilitoa maagizo 10 na kati ya hayo ni mawili tu yametekelezwa na katika Halmashauri ya Mbinga Mji kati ya maagizo matano yaliyotolewa hakuna agizo hata moja lililotekelezwa.

"Hali ya utekelezaji wa maagizo ya LAAC hairidhishi kabisa, katika Halmashauri za Mbinga Mji na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga hakuna hata agizo moja ambalo limetekelezwa na kufungwa hadi sasa, kwa nini maagizo hayo yote bado hayajafungwa?",alihoji.

Kanali Abbas pia alielezea mwenendo wa ushughulikiaji wa Hoja na Mapendekezo ya CAG katika halmashauri hizo tatu, bado hauridhishi ambapo amewaomba Waheshimiwa Madiwani kufuatilia kwa karibu na kuhakikisha hoja zinajibiwa ipasavyo na kuhakikisha kuwa hoja hizo hazijirudii tena.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Mkoa aliiagiza Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na uongozi wa halmashauri kupitia majibu na vielelezo vyote kabla ya kuwasilisha kwa CAG kwa ajili ya uhakiki.

Pia aliziagiza halmashauri hizo kuchukua hatua mapema za kinidhamu kwa watumishi wanaozalisha hoja au wanaosababisha hoja zilizoshindikana kujibiwa.

Katibu Tawala Mkoa wa Ruvuma, Rehema Madenge, akizungumza kwenye kikao hicho, alisema hoja zote zilizoagizwa na LAAC zimetokana na utekelezaji wa shughuli kwenye Halmashauri husika, hivyo Halmashauri zinahusika moja kwa moja kujibu hoja hizo.

Amesisitiza kuwa hoja hizo zilizoibuliwa zina majibu, hivyo amewaagiza watendaji hao kuhakikisha wanajibu hoja zote ili zifungwe na kuweka mkakati thabiti wa kuhakikisha hoja hizo hazijitokezi tena.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mbinga, Deusderius Haule, alimhakikishia mkuu wa mkoa kuwa atasimamia kikamilifu kuhakikisha wanatekeleza maagizo ya kujibu hoja za LAAC na kutekeleza mapendekezo ya CAG.

HADITHI

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani.
Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-6

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




Ndani ya basi pamoja na kwamba Kamal na Mariamu walikuwa gumzo, walikuwa pia kivutio, kwani mara kwa mara walikuwa wanabadilishana kukaa dirishani hadi basi lilipofika Stendi ya Basi ya Magufuli.

"He! Yaani tumekuwa wote tunaongea tangu Bwawani, lakini nilikuwa bado sijakuuliza jina hadi tunafika!" Mariamu akaangua kicheko, halafu akamwambia. "Yaani unaongea na mtu humjui jina? "Naye akauliza kiutani akiendelea kucheka."

Walikuwa ndiyo kwanza wanateremka kwenye basi, halafu ilionekana kama wanaelekea sehemu moja wakati sivyo.

Abiria wote ndani ya basi hilo wakaamini ule msemo wa 'wagombanao ndiyo wapatanao.' Kwa sababu walishuhudia kwa macho yao, watu wawili wakigombana ndani ya basi wakati linaondoka Stendi ya Basi Msamvu, Morogoro, lakini wanateremka wakiwa pamoja, wakiongea kwa bashasha kwenye Stendi ya Mabasi ya Magufuli.

"Kwani na wewe unanijua jina?" Kamal akamuuliza.

"Mhh! Sikujui kwa kweli."

"Sasa kwa nini unanicheka mimi kutojua jina lako. Mimi naitwa Kamal."

"Mimi naitwa Mariamu."

"Okay, jina zuri kama wewe mwenyewe!"

Walisaidiana kutoa mabegi kama vile walikuja pamoja. Yoyote ambaye alikuwa kituoni pale, au ameshuka kwenye basi lingine akawaangalia, anaweza kudhani wametoka sehemu moja. Walipanda pamoja, na mwingine akaenda mbali zaidi na kusema ni mtu na mpenzi wake au mkewe.

Waliokuwa ndani ya basi lile ndiyo waliokuwa wanajua kila kitu. Kilichotokea huko, na wanachokiona sasa ni vitu viwili tofauti.

Walitoka taratibu wakiwa wameongozana, wamependezana, wakiongea kwa furaha kama hakuna kilichotokea.

Kwa muda huu tu mfupi, alichogundua Mariamu ni kwamba Kamal alikuwa mwanaume mwema, mpole, mcheshi na anayeonekana mwenye misimamo. Moyoni alimhusudu. Aliona akipata mwanaume kama yule anayeonekana kujiamini basi atakuwa amepata kitu cha thamani sana kwenye maisha yake.

"Sasa bibie wewe unaelekea wapi?"

**"Ukweli unabaki pale pale kuwa mimi nilipanda hili basi, nikachagua ile siti, nikakaa dirishani, kwa sababu lilikuwa lina abiria wachache nikaamua kuteremka kwanza ili kupunga upepo na kunyoosha kidogo miguu kwa sababu nilijua nikirudi nitakaa hapo kwa muda mrefu, kumbe wewe ukapanda na kwenda kukaa kwenye ile siti, sasa abiria walikuwa wanasubiri udhaifu wa mwanaume, nashukuru hakuuona, ndiyo maana walishangaa sana."**

Akauliza.

"Mimi naishi Tabata."

"Okay vizuri."

"Na wewe unakaa wapi?"

"Mimi naishi maeneo ya Kinondoni Studio, karibu sana nyumbani kwangu."

"Ahsante na wewe pia karibu kwangu."

"Mhh, sipigwi huko? Maana mimi naogopa sana kupigwa." Kamal akatania.

Mariamu akacheka kicheko ya kimbea cha kike. Kikali na kifupi. "Inzi kufia kwenye kidonda halali yake."

Ni wakati ambao Kamal aligundua kuwa baadhi ya watu ha sa wanaume walikuwa wanawaangalia sana. Na walichikuwa wakishangaa ni uzuri wa msichana aliyekuwa naye.

Tayari walikuwa nje ya kituo cha mabasi cha Magufuli.

"Ngoja nichukue simu yangu nikuitie gari kwenye mtandao ikutoe hapa uende nyumbani, mwisho watu watatuzunguka hapa, maana wanatushangaa hao," Kamal alimwambia Mariamu ambaye alikuwa kama vile hajui kinachoendelea.

Taxi iliyoitwa kwenye mtandao ilipofika, Kamal na Mariamu walisaidiana kuweka mizigo kwenye buti, wakaagana na kukumbatiana.

"Tutawasiliana rafiki." Kamal alimwambia. Hakutaka kutumia neno mpenzi kwa sababu ni mapema mtu na ilikuwa bado hajamtamkia rasmi, na muda ulikuwa bado mfupi kufanya hivyo.

"Na wewe ukifika nyumbani, niambie kama utakuwa umefika salama." Mariamu alisema huku akiwa tayari kufunga mlango.

"Nitafanya hivyo."

******************************

Ndivyo Kamal alivyoweza kuopoa chombo hicho kinachotetemesha watu na pesa zao, lakini wasiweze kumpata.

Maduka yake mawili ya vipodozi, Tabata na Buguruni, saluni ya kike Ilala na ya kiume Mtoni, ni vitega uchumi ambavyo vinamuingizia pesa zinazomtosha kabisa kuendesha maisha yake na kusaidia hata ndugu zake, bila kutegemea mtu yoyote.

Hakuwa na tamaa yoyote ya kuwa na mwanaume tajiri, cheo kutokana na kile alichowahi kuambiwa na mama yake, lakini pia aliona kama anaweza kukosa uhuru wake.

Akaendelea kujitazama kwa mara ya nne kioo.

Kumbe hata wanaume wanavyotukanana, kupigana na hata kutishia kuuana walikuwa sahihi.

"Wana haki, maana si kwa uzuri huu." Akajiambia mwenyewe akiwa anajitazama kwa mara nyingine tena kwenye kioo kikubwa kilicho mbele yake.

Ni mwanamke ambaye kila mwanaume alitamani kuwa naye. Sura yake ya mviringo, rangi yake maji ya kunde, mashavu ambayo yalikuwa na vishimo ambavyo vilijidhihirisha wazi pale anapocheka.

Uzuri wake hapo unaongezeka kwa mwanya, uliojiegemeza kwenye mpangilio mzuri na meno maupe kama theluji.

Pua yake ilikuwa mchongoko, na kushoto kwake kiliota kidoti cheusi ambacho kiliendelea kuupamba urembo wa msichana huyo.

Macho yake peupe ya duara malegevu, yaliwafanya wanaume kuona kama yanawaona hadi ndani ya mioyo yao.

Alikuwa na umbile namba nane, hipsi zilionekana vizuri, na nyuma ya sura yake alikaa vizuri na kuwa kivutio si kwa wanaume tu bali hata kwa wanawake wenzake.

Nao walikuwa wakimuona walikubali kuwa pamoja na kwamba nao ni warembo, lakini mwenzao amependelewa.

Mwili wake pia ulikubali nguo yoyote aliyoivaa. Ilikuwa ni saa 1:00 usiku, baada ya kutumia karibuni dakika 20 nzima kuvaa, aliendа kujiangalia tena kwenye kwenye kioo na kuridhika kuwa sasa anaweza kutoka.

Alikuwa anakwenda kukagua na kuchukua mahesabu ya pesa kwenye vitega uchumi vyake.

Alipotoka nyumbani mlangoni, akakata upande wa kulia ambako kulikuwa na njia ya kwenda barabarani ambako angechukua bodaboda.

Ghafla akahisi kama kuna kitu au mtu nyuma yake. Kabla hajageuka kutazama kuna nini alipigwa na kitu kizito kichwani.

Alichoona hapo mwanzo ni nyota nyota nyingi nyekundu, baadaye giza totoro. Kilichofuata akahisi kutumbukia kwenye shimo kubwa ambalo halikuwa na mwisho.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# TABORA UNITED YAKABIDHIWA KWA MKUU MPYA WA MKOA

**Na Adam Fungamwango**

MKUU wa mkoa mpya wa Tabora, Paul Chacha amekabidhiwa rasmi timu ya mpira wa miguu ya Tabora United kutoka kwa mkuu wa zamani, Batilda Buriani, aliyehamishiwa mkoani Tanga.

Katika hafla ya makabidhiano iliyofanyika juzi mkoani Tabora, Batilda amemwambia mkuu wa mkoa huyo kuwa amemkabidhi timu hiyo ili kushughulikia changamoto ilizonazo ili kuitoa kwenye hali mbaya kwenye msimamo wa Ligi.

"Changamoto bado tunayo ya kuinyanyua timu ipo sehemu ambayo si nzuri, kuwa na basi la la timu, kujenga morali ya mashabiki ili ikicheza nyumbani ijione ipo nyumbani," alisema Batilda.

**Aidha, alimtaka mkuu huyo kusimama kidete ili kufanyike uchaguzi wa chama cha soka mkoani humo.**

Akizungumza baada ya kukabidhiwa timu hiyo, Chacha alisema atafanya yote aliyoelekezwa na mengine ambayo ataona yanafaa kufanywa kwa ajili ya manufaa na faida ya timu na mashabiki wa soka mkoani humo.

"Nitafanyia kazi changamoto zilizopo na kuondoa migogoro midogo midogo iliyoo ndani ya klabu yetu," alisema Chacha.

Batilda ambaye anaenda kuwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga ataenda kukutana na kuisimamia timu za mkoa huo ikiwemo Coastal Union inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Ila ndugu yangu Chacha ujue sasa una ushindani na mimi nakwenda kuibeba Coastal Union katika kituo changu kipya cha kaza, Tanga na kwa kuwa timu zote zinacheza Ligi Ku badi tutakutana tu," alisema Batilda.

Tabora united ipo nafasi ya 13 katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 21, imecheza michezo 21, imeshinda michezo minne, imetoa sare michezo tisa na kufungwa michezo minane.



Balozi wa kampuni ya Betika, Baraka Mpenja (kulia) akimkabidhi simu aina ya iphone 15, Antony Peter Longolongo (katikati) ambaye aliibuka mshindi wa kwanza kwenye kampeni ya Mtoko wa Kibingwa kushoto ni Ofisa habari wa kampuni hiyo, Juvenalius Rugambwa.**PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# *Mtoko wa Kibingwa dabi Ligi Bara wafikia patamu*

**Mwandishi Wetu**

Habari ya mjini ni matokeo ya jana ya Simba na mechi ya leo ya Yanga kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, hata hivyo mashabiki wa timu hizo wanajambo lao kwenye kampeni ya 'Mtoko wa Kibingwa' kuelekea kwenye mechi nyingine ya dabi itakayowakutanisha vigogo hao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Baada ya mechi za kimataifa za timu hizo, sasa upinzani wao utahamia kwenye Ligi ambako Yanga inaongoza msimamo ikifuatiwa na Azam kisha Simba, uhondo zaidi ni kwenye dabi ya mzunguko wa pili ya Ligi Kuu msimu huu Yanga ikiwa mwenyeji wa Simba.

Mechi hiyo, mbali na Kampuni ya michezo ya kubashiri matokeo ya Betika kuwapa fursa mashabiki 56 kuishuhudia mubashara katika hadhi ya VIP kwa gharama za kampuni hiyo, pia wanatoa zawadi za wiki na za mwezi kwa washindi mbalimbali.

Miongoni mwa zawadi hiyo ni simu mpya ya iphone 15 ambayo inatolewa kwa mshindi mmoja kila mwezi na simu nyingine janja za tecno kwa washindi wawili kila wiki.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Ofisa Habari wa Betika, Juvelinaus Rugambwa amesema tayari mshindi wa kwanza wa iphone 15 amepatikana na juzi amekabidhiwa zawadi yake katika droo ya Mtoko wa Kibingwa.

Alimtaja mshindi huyo kuwa ni Peter Longolongo wa Gongo la Mboto, Dar es Salaam aliyekabidhiwa zawadi hiyo na mdau wa michezo, Baraka Mpenja ambaye ni balozi wa Betika.

"Kampeni itafanyika kwa miezi miwili, bingwa wa pili wa iphone 15 atatangazwa Aprili 9 ambapo tutakamilisha mwezi wa pili wa kampeni hii kuelekea kwenye dabi ya Simba na Yanga itakayofanyika katikati ya Aprili," alisema Rugambwa.

Akizungumzia kampeni hiyo, Rugambwa alisema mbali na zawadi za wiki na za mwezi, kubwa kuliko ni mashabiki 56 ambao watashuhudia bure dabi hiyo.. "Kila wiki tumekuwa na washindi wanane watakaopata fursa hiyo, lengo ni kuwapa fursa mashabiki wa Simba na Yanga kuishuhudia dabi hiyo mubashara kwa hadhi ya VIP kwa gharama za Betika," alisema Rugambwa.

Alisema washiriki wote wataingia kwenye droo kubwa ya kutafuta nafasi ya kuishuhudia dabi hiyo ya watani wa jadi mubashara.

Akizungumzia droo hiyo tangu imeanza, Rugambwa alisema imeweza kuwaleta mashabiki 350 kushuhudia dabi hiyo tangu ilipoanza.

"Wengi hawakuwa wamewahi kuishuhudia dabi hiyo mubashara, jambo hili limewakutanisha na wachezaji wanaowapenda na kuwaona wakicheza.

"Bila kujali kama mkeka utachanika au la, kila atakayebashiri nasi ataingia kwenye droo ya Mtoko wa Kibingwa yenye kauli mbiu ya 'Kaa kwa Kutulia', wakijiandaa kuiangalia dabi hiyo kwa hadhi ya kipekee" alisema.

## SHIMUVUTA yaandaa rasimu kanuni fedha

**Na Shufaa Lyimo**

KAMATI ya Utendaji ya Shirikisho la Michezo ya Vyuo vya Elimu ya Juu Tanzania (SHIMIVUTA) imeanza maandalizi ya kuandaa rasimu ya kanuni za fedha pamoja na mpango wa maendeleo yake.

Utekelezaji huo ni maelekezo ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk Damas Ndumbaro aliyoyatatoa katika kikao cha viongozi wa vyama na Mashirikisho ya michezo kilichofanyika mapema mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, mara baada ya kumaliza kikao hicho mjini Bagamoyo Rais wa SHIMIVUTA Juhudi Samu, alisema kuwa watahakikisha kanuni za fedha za Shirikisho hilo zinaendana na za Baraza la Michezo la Taifa (BMT) ili kuepusha mianya ya utakatishaji fedha za Shirikisho hilo.

Alisema kuwa mashirikisho yamekuwa yakipata fedha kutoka kwa wadhamini isipokuwa wanazitumia tofauti na maombi waliyoyaomba.

"Tunaendelea kufanyia kazi maelekezo ya waziri ili tukamilishe kanuni na kuandaa mpango wa maendeleo wa Shirikisho ambao tukiukamilisha tutauwasilisha katika chombo husika tukiwa tunajipanga kuwasilisha katika kikao cha vyama na mashirikisho ya michezo kitakachofanyika Juni mwaka huu jijini Dodoma," alisema Samu.

Aidha, Rais huyo alisema miongoni mwa mambo waliyojadili katika kikao hicho ni pamoja na kuandaa kalenda ya mwaka, bajeti ya mwaka huu, kuandaa kanuni zitakazosimamia mashindano ya mwaka mzima.

## Ngumi taifa waingia kambini

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha timu ya Taifa ya ngumi "Faru Weusi wa Ngorongoro" kinatarajia kuingia kambini leo kujiandaa na mashindano ya Mandela yatakayofanyika Aprili 15 hadi23 mwaka huu Durban, Afrika ya Kusini.

Wachezaji wa timu hiyo walipewa mapumziko ya siku mbili baada ya kurejea nchini kutoka kwenye mashindano ya Afrika yaliyofanyika nchini Ghana.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo Samweli Kapungu, alisema wanaendelea vema na mazoezi kuhakikisha wanakwenda kufanya vizuri kwenye mashindano hayo.

Alisema wanataka kutumia mashindano hayo kupata medali za dhahabu ambazo walishindwa kuzipata kwenye michuano ya Afrika.

"Malengo yetu ni kwenda kushindana ili tupate medali za dhahabu ili kulipa heshima Taifa letu pamoja na kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan," alisema Kocha huyo.

Aidha, aliongeza kuwa anaendelea kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza kwenye mashindano ya Afrika ili yasijirudie kwenye mashindano hayo ya Mandela.

Aliwataka watanzania pamoja na wadau mbali mbali wa mchezo wa ngumi kuwaunga mkono wakatimize mipango yao.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**FRANK ATAKIWA MAN UNITED**
KLABU ya Manchester United inamlenga kocha wa Brentford, Thomas Frank kuchukua mikoba ya Erik ten Hag pale Old Trafford msimu wa joto, na sio kocha wa England, Gareth Southgate ***(Football Transfers)***

**WERNER MKATABA WA KUDUMU**
TOTTENHAM Hotspur wana nia ya kukamilisha mkataba wa kudumu kwa mshambuliaji wa RB Leipzig na Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 28, lakini wanaripotiwa kuwa hawana haraka ya kuanzisha kipengele cha kumnunua kwa pauni milioni 14.5. ***(Four Four Two)***

**DIOMANDE KUTUA ARSENAL**
ARSENAL imefikia ofa ya pauni milioni 51 pamoja na bonasi ambayo Chelsea wametoa kwa Sporting Lisbon kwa mlinzi wa Ivory Coast, Ousmane Diomande mwenye umri wa miaka 20. (***Record***)

**HAALAND NA FURSA**
MSHAMBULIAJI wa Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 23, anaitazama robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ya Manchester City dhidi ya Real Madrid kama fursa ya kuthibitisha uwezo wake wa kuhamia miamba hao wa Hispania. (***AS - kwa Kihispania)***

**BENRAHMA KUSAINI LYON**
KLABU ya West Ham inatarajia winga wa Algeria mwenye umri wa miaka 28, Said Benrahma kusaini mkataba wa kudumu katika klabu ya Ligue 1 ya Lyon msimu huu wa joto.(***Football Insider)***

**LUKJANCIKS ATAKIWA LEVERKUSEN**
BAYERN Leverkusen ni miongoni mwa Klabu za juu za Ulaya zinazotaka kumsajili mlinda lango wa Everton na England, Douglas Lukjanciks mwenye umri wa miaka 16. (***Mail)***

**ZERBI HANA HARAKA**
KOCHA wa Brighton, Roberto de Zerbi amefurahishwa na nia ya Bayern Munich kutaka huduma yake, lakini kocha huyo wa Italia hana haraka ya kufanya uamuzi juu ya mustakabali wake wa muda mrefu.(***Mirror)***

**CHELSEA KUADHIBIWA**
CHELSEA inakabiliwa na adhabu ikiwa ni pamoja na kukatwa pointi kwenye Ligi Kuu England iwapo itapatikana na hatia ya kukiuka sheria za matumizi chini ya umiliki wa Roman Abramovich. (G***uardian)***

**L'POOL, MAN ZAMGOMBEA CHIESA**
LIVERPOOL itachuana na Manchester United kumnunua fowadi wa Juventus raia wa Italia, Federico Chiesa mwenye umri wa miaka 26. (***Teamtalk***)

**TOULOUSE KUNUNULIWA**
WAMILIKI wa Liverpool, Fenway Sports Group na mkuu mpya wa soka, Michael Edwards wanaangalia mpango wa kuinunua klabu ya Toulouse ya Ligi Kuu ya Ufaransa. (***Football Insider***)

**CANCELO KUONGEZEWA**
BARCELONA inaangalia uwezekano wa kuongeza muda wa mkopo wa beki wa pembeni wa Ureno, Joao Cancelo mwenye umri wa miaka 29 kutoka Manchester City kwa mwaka mwingine. (***Marca***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# DI MARIA ATISHIWA KIFO

### Wafanyakazi wa nyumba yake wakutana na ujumbe uliokuwa na vitisho kama nyota huyo atacheza kwenye....

**ROSARIO,** Argentina

POLISI wa Argentina wanachunguza vitisho vya kifo vilivyotolewa kwa familia ya mshambuliaji Angel Di Maria nyumbani kwao Rosario.

**Wafanyakazi kwenye nyumba ya staa huyo mshindi wa Kombe la Dunia na Argentina mwaka 2022, walisema waliku tana na ujumbe uliokuwa na vitisho vya vifo kama ataendelea na mpango wa kutaka kucheza kwenye moja ya klabu katika mji wa Rosario.**

Winga huyo mwenye umri wa miaka 36 wa Benfica ya Ureno hivi karibuni alisema anaweza kurejea kucheza kwenye klabu yake ya utoto ya Rosario Central.

"Vitisho kama hivi vinasababisha usumbufu mwingi kwenye jamii na hilo ndio lengo lake, kufanya wananchi wawe na hofu, kuwatisha watu muhimu kwenye jamii," alisema Esteban Santantino, anayefanya kazi kwenye vyombo vya usalama katika mji wa Rosario.

Vyombo vya habari vinasema malengo ya vitisho hivyo bado hayako wazi, ingawa Polisi walishindwa kukataa taarifa zozote za uchunguzi.

Di Maria juzi alianza kwenye mchezo wa kirafiki wa kimataifa dhidi ya Costa Rica.

Rosario imekumbwa na matukio ya vurugu nyingi miongoni mwa magenge yanayohusika na uuzaji wa dawa za kulevya.

## HABARI MICHEZO

# MAN CITY VS ARSENAL MECHI YA UBINGWA EPL




**MANCHESTER,** England

MBIO za Arsenal kuelekea ubingwa wa Ligi Kuu ya England zitatoa taswira halisi kesho Jumapili wakati watakapocheza na Manchester City huku wakitaka kupata ushindi wao wa kwanza katika dimba la Etihad tangu 2015.

Hitimisho la mapumziko ya kimataifa ya Machi inaashiria kuanza kwa mchujo, na huu ni mchezo wa mwisho wa kumenyana kati ya wawaniaji watatu wa taji la EPL.

Ni pambano kubwa, na mshindi atakuwa na hisia zisizobadilika za kasi kuelekea wiki chache za mwisho za msimu.

Ndoto ya Arsenal ya kutwaa ubingwa ilizimwa jijini Manchester katika msimu uliopita walipochapwa na wapinzani wao hao.

Hata hivyo, kuna makali kwa Washikabunduki hao wakati huu, na rekodi yao katika mechi kubwa msimu huu inawaweka katika nafasi nzuri kuelekea kwenye pambano la Jumapili.

City wana majeruhi kadhaa baada ya mapumziko ya kimataifa, kama ilivyo kwa Arsenal, ingawa timu zote zinatarajiwa kuwa karibu na nguvu kamili.

Ushindi kwa Arsenal kwenye mchezo huu ndio itakuwa hakikisho la mbio zao kwenye ubingwa.

**MAJERUHI**

Man City wana wasiwasi mwingi kuelekea mechi ya Jumapili kutokana na majeruhi.

Kyle Walker anasemekana kuwa 50/50, kama John Stones, huku Manuel Akanji ameripotiwa kuwa sawa.

Ederson anatarajiwa kurejea mapema kuliko ilivyotarajiwa kutokana na jeraha la paja, huku Kevin De Bruyne na Jack Grealish wote wakifanya mazoezi kabla ya mchezo.

Kwa upande wa Arsenal Gabriel Martinelli, bado kuna shaka ya kucheza kutokana na jeraha la mguu.

Mbrazil huyo anakabiliwa na kinyang'anyiro cha kuwa fiti wikendi hii, na kuna uwezekano ataingia kwenye benchi ikiwa atasafiri na kikosi.

Bukayo Saka alijiondoa kwenye majukumu ya kimataifa kutokana na jeraha dogo la misuli, lakini winga huyo anatarajiwa kuwa fiti kwa ajili ya safari ya Etihad.

Jurrien Timber anakaribia kurudi, lakini hii inaweza kuja mapema sana kwa Mholanzi huyo. Thomas Partey na Takehiro Tomiyasu wote watakuwa kwenye kikosi cha siku ya mechi.

Vikosi

Man City: Ederson; Walker, Akanji, Dias, Ake; Rodri, De Bruyne, Kovacic; Bernardo, Haaland, Grealish.

Arsenal: Raya; Nyeupe, Saliba, Gabriel, Kiwior; Mchele, Jorginho, Odegaard; Saka, Havertz, Trossard.

# *Liverpool yajitoa kwa Alonso*

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL imeachana na mpango wa kumtaka kocha wa Bayer Leverkusen, Xabi Alonso kuchukua nafasi ya Jurgen Klopp, kwa mujibu wa ESPN, huku Roberto De Zerbi wa Brighton na kocha wa Sporting CP Ruben Amorim wakichukuliwa kuwa wagombea wanaoongoza kwa kazi hiyo ya Anfield.

Alonso, mshindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa mchezaji wa Liverpool mwaka 2005, yuko mbioni kuiongoza Leverkusen kutwaa taji lao la Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, msimu huu.

Klopp alitangaza hadharani Januari kwamba atajiuzulu kama kocha wa Liverpool msimu huu wa joto.

Kocha huyo wa zamani wa Borussia Dortmund aliifahamisha klabu kuhusu nia yake Novemba mwaka jana na Alonso aliibuka kama mwenye nafasi kubwa kuhamia Anfield kwa sababu ya uhusiano wake na timu hiyo aliyoichezea.

Huku Bayern Munich pia wakitafuta kocha mpya kutokana na Thomas Tuchel kuondoka Allianz Arena mwishoni mwa msimu huu, Alonso pia alikuwa ameibuka kama mgombeaji mkuu wa kazi hiyo kule Bavaria. Alonso pia aliichezea Bayern wakati wake wa uchezaji.


Rais wa heshima wa Bayern, Uli Hoeness alisema Alhamisi kwamba kumwajiri Alonso msimu huu wa joto "labda haiwezekani," na sasa vyanzo vya Liverpool vimeiambia ESPN kwamba klabu imechagua kufuata malengo mengine kwa sababu ya kuelewa kuwa Alonso yuko tayari kubaki Leverkusen kwa angalau msimu mmoja zaidi.

Vyanzo vya habari vimesema kuwa Michael Edwards, ambaye alirejea Liverpool kama Mkurugenzi Mtendaji wa klabu hiyo mapema mwezi huu akiwa mkurugenzi wa michezo, tayari alikuwa amebainisha chaguo mbadala kwa Alonso.

De Zerbi, ambaye timu yake ya Brighton itasafiri hadi Anfield kwenye Ligi Kuu England kesho, ana uungwaji mkono mkubwa ndani ya uongozi wa Liverpool.

Wakati rekodi ya De Zerbi katika klabu ya Brighton imemtambulisha kama kipenzi kipya, kocha wa Sporting, Amorim pia anaonekana kuwa mshindani wa kweli kumrithi Klopp.

Wakati huo huo, Real Madrid wanatarajiwa kutupa ndoano ya kumchukua Alonso wakati mkataba wa Carlo Ancelotti utakapomalizika 2026.



# Manchester United haina haraka kwa Mainoo

**MANCHESTER,** England



MANCHESTER United haina haraka ya kumpa mkataba mpya kiungo wa kati, Kobbie Mainoo ingawa mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2028.

Mainoo mwenye umri wa miaka 18 hivi karibuni amekuwa akianza kikosi cha kwanza na kumwezesha kuitwa kikosi cha timu ya Taifa ya England chini ya kocha, Gareth Southgate kwenye mchezo dhidi ya Brazil na Ubelgiji.

Mainoo alisaini mkataba Februari 9, 2023 alipocheza kwa mara ya kwanza kwenye kikosi cha kwanza, akitia saini mkataba wa miaka minne na chaguo la miezi 12 zaidi.

Hali yake imebadilika sana tangu wakati huo. Lakini gazeti la Manchester Evening News limeripoti kuwa, licha ya mazungumzo ya awali kuhusu mkataba mpya, klabu hiyo haina haraka.

Mainoo mwenyewe hafikiriwi kutanguliza mkataba mpya pia, na mkataba wake uliopo tayari unafikiriwa kujumuisha motisha zinazohusiana na uchezaji.

Kiungo huyo ni muhitimu wa akademi ya Man United, amecheza mechi 15 za Ligi Kuu England katika maisha yake ya soka hadi sasa.

Bao lake la kwanza katika mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Wolves Februari, lilipewa tuzo ya bao bora la mwezi la Ligi Kuu na kuwahakikishia Mashetani Wekundu kupata ushindi wa dakika za mwisho.

Kupanda kwake kumekuwa kwa kasi, na tangu afanye vizuri kwenye Uwanja wa Goodison Park wakati United iliposhinda 3-0 dhidi ya Everton Novemba mwaka jana, Mainoo amekuwa kipenzi cha Erik ten Hag uwanjani.

Kuna uwezekano wa kuwa na mabadiliko mengi Old Trafford majira ya joto, huku timu ikitafuta kusajili wachezaji wapya na kujua mustakabali wa muda mrefu wa meneja.

HABARI MICHEZO

## Yanga, Mamelodi mechi ya kisasi

INATOKA UKURASA 24

Koussi, Joyce Lomalisa, Stephen Aziz Ki na safu ya ushambuliaji kuna Guede, Clement Mzize na Kennedy Musonda najua kila mmoja na uwezo wake, hatuwaogopi bali tunawaheshimu Yanga," alisema Mokwena.

## Ajali yaua shabiki Simba, Yanga yatoa pole

INATOKA UKURASA 24

ambayo imetokea maeneo ya Doma Mkoani Morogoro, ikiripotiwa mtu mmoja kujeruhiwa huku kukiwa hakuna madhara makubwa zaidi.

Uongozi wa Simba jana asubuhi umetoa taarifa rasmi kuhusiana na ajali hizo, huku baadhi ya viongozi wakiwa wameelekea eneo la ajali, Vigwaza kwa ajili ya kutoa msaada zaidi kwa waathirika.

"Uongozi wa klabu ya Simba umepokea kwa masikitiko taarifa za ajali za mashabiki wetu silizotokea usiku wa kuamkia leo wakiwa njiani kuelekea Dar es Salaam kushuhudia mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly,"

"Ajali ya kwanza imehusisha mashabiki wa tawi la Kiwira Rungwe la mkoani Mbeya ambapo taarifa za awali za Jeshi la Polisi zinasema mtu mmoja amepoteza maisha.

Ajali ya pili ni Tawi la Wekundu wa Border kutoka Tunduma iliyotokea Doma, mkoani Morogoro, ambapo taarifa kutoka eneo la tukio linasema hakukuwa na madhara makubwa zaidi ya mtu mmoja kuumia," ilisema sehemu ya taarifa ya uongozi wa Simba.

Baada ya ajali hizo, klabu ya Yanga ilitoa taarifa ya kuwapa pole watani zao wa jadi, huku ikiwataka madereva wote wanaobeba mashabiki wa soka wanaokwenda kungalia mpira kuwa watulivu barabarani na kuzingatia alama za usalama wakati wote wa safari.

"Uongozi wa Klabu ya Yanga, unatoa pole kwa uongozi wa Simba kufuatia msiba wa shabiki wa timu hiyo aliyefariki dunia usiku wa kuamkia leo (jana), kwenye ajali ya gari lililobeba mashabiki waliokuwa njiani kuja Dar es Salaam kutazama mchezo wa robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tunaomba Mwenyezi Mungu aipumzishe roho ya marehemu mahala pema peponi, pia uongozi unatoa pole kwa wote waliopata majeraha kwenye ajali mbili zilizotokea maeneo ya Vigwaza Pwani na Doma, mkoani Morogoro wapone haraka na kurejea kwenye majukumu yao," ilisema taarifa hiyo ya Yanga.

# WACHEZAJI, KENGOLD, BIASHARA, WAGOMBEA KIATU CHA DHAHABU

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi ya 'Championship' ikielekea ukingoni, wachezaji Edger William wa KenGold na Boban Zirintusa wa Biashara United,wanafukuzana kuwania tuzo ya ufungaji bora.

Edger, anaongoza kwa kupachika mabao kwenye ligi hiyo akiwa amefunga 17, na kuiwezesha timu yake ya KenGold kuongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 60, ikihitaji pointi sita tu kuweza kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara kwa ajili ya msimu ujao.

Zirintusa, raia wa Uganda ambaye ameshacheza klabu mbalimbali za Ligi kuu, ikiwemo, Mtibwa Sugar anamfukuza kwa karibu Edger akiwa na mabao 16 ambayo yameiwezesha Biashara United kuwa kwenye nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo, ikiwa na pointi 53, ikipigania moja ya nafasi mbili za juu za kupanda moja kwa moja moja.

Oscar Mwajanga wa Mbeya Kwanza anashika nafasi ya tatu kwenye orodha hiyo ya wafungaji akiwa na mabao 14, huku Frank Francis wa TMA na Maulid Shaaban wa Mbeya Kwanza wote wote wakiwa na mabao 13.

Jumla ya wachezaji watano wamepachika mabao tisa kila mmoja, ambao ni Ramadhani Kapera wa Mbeya Kwanza, Salim Aiyee Mbuni FC na sasa amesajiliwa na Coastal Union iliyopo Ligi Kuu, winga wa zamani wa Simba, Haruna Chanongo wa Pamba, Abdulaziz Shahame wa TMA na Kilaza Mazoea wa Cosmopolitan.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Maktaba wakiwania mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika viwanja vya kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *KMC yaingia kambini kuiwinda Prisons*

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha KMC kimeingia kambini tayari kwa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya mapumziko ya siku kadhaa ya michezo ya kirafiki ya kalenda ya FIFA.

Mchezaji mwandamizi wa timu hiyo, Andrea Vicent amesema yeye wachezaji wenzake wameingia kambini na kuanza mazoezi ajili ya kujiwinda na mechi yao dhidi ya Tanzania Prisons utakaochezwa Aprili 12 kwenye Uwanja wa Sokoine, jijini Mbeya.

"Tumerejea na wachezaji wenzangu, lengo ni kuipigania timu yetu ili imalize msimamo ikiwa sehemu nzuri na msimu huu lengo letu ni kumaliza nne bora," alisema mchezaji huyo wa zamani wa Yanga.

Mchezaji mwingine Awesu Awesu alisema mbali na kwamba hawakuanza vizuri mwaka huu, lakini baada ya kuichapa Tabora United mabao 4-2, wamekuwa na morali kubwa ya kupambana na anaamini watafikia malengo waliyoyakusudia.

"Malengo yetu ni kucheza michuano ya kimataifa msimu ujao, dhamira ipo na tumeshawahi kufanya hivyo," alisema Awesu.

KMC inashika nafasi ya sita katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 28 baada ya kucheza michezo 21, ikishinda michezo minane, imetoka sare michezo sita na kufungwa michezo saba.

Imebakisha michezo tisa msimu huu, ambapo baada ya kucheza dhidi ya Prisons, itacheza dhidi ya Mtibwa Sugar, Uwanja wa Manungu Complex, Morogoro Aprili 16, dhidi ya Dodoma Jiji, Aprili 28 kwenye uwanja wa Jamhuri Dodoma na Mei 2, itakuwa Uwanja wa Lake Tanganyika kucheza na wenyeji, Mashujaa FC.

Baada ya hapo itakuwa na kibarua kingine Mei 8, nyumbani dhidi ya Kagera Sugar, Azam na Singida Fountain Gate, kabla ya kucheza na Simba Mei 20, na Mei 29 kumalizana na Coastal Union.

Michezo
Jumamosi Machi 30, 2024
Nipashe



Liverpool yajitoa kwa Alonso UKURASA 22




Ronwell




Diarra

## Ajali yaua shabiki Simba, Yanga yatoa pole

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba ikicheza mechi yake ya kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika jana dhidi ya Al Ahly ya Misri, imepata pigo baada ya mashabiki wake kujeruhiwa na mmoja kufariki dunia, katika ajali mbili tofauti zilizotokea usiku wa kumkia jana wakati wakielekea Dar es Salaam kutazama mechi hiyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Pius Lutumo amethibitisha kutokea ajali maeneo ya Vigwaza mkoani humo ikihusisha gari aina ya Toyota Coaster iliyowabeba mashabiki wa klabu hiyo Tawi la Kiwila mkoani Mbeya na Lori.

"Ni kweli imetokea hiyo ajali imesababisha kifo cha mtu mmoja na majeruhi watatu, taarifa nyingine tunaendelea kuzifuatilia na taarifa zaidi tutawapatia baadaye," alisema Lutumo.

Shuhuda wa ajali hiyo ambaye pia ni shabiki wa Simba, Kassim Hassan kutoka Tawi la Wekundu wa Dodoma amesema wameshuhudia ajali hiyo wakiwa njiani kwenye gari lingine, wakienda Dar es Salaam kutazama mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kati ya timu hiyo na Al Ahly, mchezo uliochezwa jana.

Ajali ya pili ni ya Tawi la Wekundu wa Boda kutoka Tunduma

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga, Mamelodi mechi ya kisasi

**Na Saada Akida**

## ●●● Wanakutana baada ya miaka 23, Gamondi ataka kazi iishie kwa Mkapa, Mokwena asema....

BAADA ya miaka 23 kupita, Yanga leo wanakutana kwa mara ya pili na mabingwa wa Afrika Kusini, Mamelodi Sundowns katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo safari hii wanakutana katika hatua ya robo fainali kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa.

**Mara ya mwisho timu hizo zilikutana kwenye hatua ya awali mwaka 2001 ya michuano hiyo ambapo katika mchezo wa kwanza Mamelodi Sundowns ilishinda kwa mabao 3-2 wakati mchezo wa marudiano uliopigwa uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, Yanga ililazimishwa sare ya mabao 3-3.**

Yanga leo wana nafasi ya kulipiza kisasi kwa wasauzi hao kwenye mchezo utakaoanza saa 3:00 usiku.

Kuelekea kwenye mchezo wa leo hatua ya makundi, Yanga wamefikia hatua hiyo baada ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye kundi D la michuano hiyo nyuma ya vinara Al Ahly ambao jana walicheza na Simba kwenye hatua hiyo ya robo fainali.

Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi ambaye amewahi kuwafundisha wasauzi hao mwaka 2006, amesema kila kitu kipo sawa na kazi iliyobaki na wachezaji wake kutimiza yake aliyowaelekeza kwenye uwanja wa mazoezi.

Gamondi alisema mchezo wa leo ni mzuri na mkubwa na lazima watumie vizuri faida ya kucheza uwanja wa nyumbani mbele ya mashabiki wao.

"Tupo tayari kwa mchezo wa kesho (leo), ni mchezo mgumu kutokana na aina ya wapinzani wetu lakini tumejipanga vizuri na tumejiandaa kukabiliana nao, kitu muhimu kwetu ni kupata ushindi," alisema Gamondi.

Aidha, amesema licha ya kuwa na majeruhi watatu kwenye kikosi chake Khalid Aucho, Yao na Kibwana Shomari pamoja na kuchelewa kujiunga na timu kwa nyota wake wawili Aziz Ki na Djigui Diarra waliokuwa kwenye majukumu ya timu zao za taifa bado watapambana kuhakikisha wanapata ushindi.

"Diarra na Aucho wamejiunga na timu jana (juzi) asubuhi na watakuwepo uwanjani leo, kukosekana kwa Aucho na Yao naamini wachezaji watakaopewa jukumu watafanya kazi vizuri kwa ajili ya timu na watanzania," alisema Gamondi.

Alisema anafahamu wana michezo miwili dhidi ya Masandawana hao, lakini kwanza anauangalia mchezo wa leo kabla ya kuanza kuipigia hesabu mchezo wamarudiano utakaochezwa Afrika Kusini Aprili 5.

"Matokeo ya mchezo wa leo yatatupa picha ni kazi kubwa kiasi gani tutakuwa nayo kwenye mchezo wa marudiano, kama kocha nataka mchezo tuumalize hapa Dar es Salaam," alisema Gamondi.

Hata hivyo mchezo wa leo utakuwa na upinzani mkubwa kutokana na kikosi cha Mamelodi chini ya kocha wake Rhulani Mokwena kuwa na kiu ya kurudia mara ya pili mafanikio yao ya kutwaa ubingwa wa michuano hiyo.

Mamelodi ikiwa chini ya kocha Pitso Mosimane ilifanikiwa kutwaa ubingwa huomwaka 2016 na msimu uliopita ilicheza hatua ya nusu fainali na kuondolewa na Wydad Casablanca.

Mlinda mlango namba moja wa timu ya taifa ya Afrika Kusini 'Bafanabafana', Ronwen Williams leo atakuwa muhimili muhimu wa Mamelodi kuzuia mipira ya washambuliaji wa Yanga.

Aidha, kurejea kwa nahodha wao Themba Zwane kunatarajia kuongeza makali yao kwenye safu ya kiungo kutokana na ubora wa nyota huyo aliyefanya vizuri akiwa na Bafanabafana kwenye fainali za Afcon zilizofanyika hivi karibuini Ivory Coast.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mokwena aliweka wazi kuwa wanaiheshimu Yanga kwa kuwa ni miongoni mwa timu kubwa Tanzania na Afrika hivyo wamechukua tahadhari zote.

"Niliwaangalia katika mchezo dhidi ya Simba na Azam FC, pia kocha wao amewahi kufundisha Mamelodi Sundowns, haitakuwa mechi tahisi lakini tumefanya maandalizi mazuri na tupo tayari kwa mchezo wetu dhidi ya Yanga," alisema Mokwena.

Aliongeza kuwa malengo yake makubwa ni kumaliza mchezo hapa Dar es salaam japo anafahamu hilo ni gumu kutokana na ubora wa wapinzani wao.

Alisema atacheza kwa tahadhari mechi ya leo kutokana na ubora na ugumu wa Yangahasa afu yao ya ulinzi huku akiwataja Ibrahim Bacca na Dickson Job kuwa ni mabeki wazuri.

"Mbali na safu ya ulinzi lakini kiungo kuna Khali Aucho, Yao

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >